# *ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA*

Asante sana Ndugu.

2 Ni vizuri sana kurudi mimbarani usiku wa leo, katika utumishi wa Bwana. Salamu maalum kwa ndugu zangu hapa juu katika—katika ninii, nyuma yangu, mimbarani. Nami nina furaha sana kuwa hapa.

3 Nashangaa yuko wapi rafiki yangu, Chris Berg? Siwezi kutambua alipo wala kumwona. Yuko wapi? Loo, wewe hapo, Chris. Kaa mbali na dubu wangu mkali. Loo! Loo, ni wakati mzuri jinsi gani mimi na Chris tulikuwa nao wakati wa mwisho huku juu. Nami nimekuwa nikimtafuta kila usiku.

4 Nami nilifanya kosa, naamini, nilisema nilikuwa nje na kula chakula cha jioni pamoja na familia ya Bonderud hapa nje, nami nikakuta kumbe si Bonderud. Nafikiri ilikuwa ni binti ya Bonderud aliyeolewa na mtu mwingine. Ninasahau, Nysted, vema, Ndugu na Dada Nysted, kama mimi . . . mko hapa, samahani, lakini wewe, nafikiri ulikuwa Bonderud kwanza kabisa. Nafikiri hiyo ni kweli. Sina hakika, lakini nafikiri hiyo ni kweli. Kwa hiyo nilikuwa nusu sawa. Lakini, hata hivyo, nilisema walikuwa wakiniua kwa ukarimu. Na hivyo karibu ndivyo ilivyoendelea. Kwa hiyo tunashukuru sana.

5 Nami nilisikia leo, kupitia kwa ndugu kutoka Dawson Creek, ninamwita Ndugu Eddie, kwamba rafiki yangu wa zamani, rafiki yetu Ndugu Durney angali hai, na kwamba, ninaamini, mmishenari mwingine kutoka huko aliniletea habari kwamba Della alikuwa ameponywa, wakati alipoweka leso hiyo kwenye titi lake, lililokuwa na uvimbe. Ninafurahia hilo sana. Nami nasikia ya kwamba Bw. Durney, akiwa mgonjwa, nami ninataka kumtembelea mara tu tutakapofika Dawson Creek, na kwenda kuzungumza naye kuhusu wokovu, na, juu ya Bwana, kwa sababu aliniahidi nilipoondoka kwamba ange—angeomba, na angemwomba Mungu amsaidie.

6 Mzee mzuri sana, ambaye ameishi tu maisha yake vichakani na kamwe hakuyawazia mambo ya Mungu hata kidogo, nadhani, lakini sasa, labda, wakati akiwa kitandani mwake kweli ninaweza kuzungumza naye sasa. Kwa hiyo, wakati mwingine inambidi Mungu kutulaza kichalichali kutufanya tuangalie juu, mwajua, kwamba, Yeye anayo njia ya kufanya mambo.

7 Lakini aliniandikia barua kuhusu binti yake, na kuniambia habari zake, na akasema alikuwa ndiye binti pekee aliyekuwa naye ambaye hakuvuta sigara na kadhalika, naye alifurahi sana

kwa ajili yake. Ndipo ndugu mwingine mmishenari kutoka huko juu akaja na kuniambia kuhusu jambo la ajabu ambalo Bwana Yesu alikuwa amewafanyia. Nami ni—ninatumaini ya kwamba Mungu ataendelea kuwa pamoja nao.

8 Sasa, wakati huu mdogo kukutana na wakati wa ushirika, sikujua kulikuwako na wahubiri wengi hivi nchini, hakika, sikujua hilo. Hilo ni sawa. Vema, nina furaha kuwaona mna viongozi wazuri, wa kiroho hapa, nao watawafundisha njia ya Bwana. Nami niko hapa kuninii, ili tu kuwa jibu kwa maombi, na kukimbia juu ya msingi waliouweka. Kukiwako sifa yoyote ya kutolewa, wapeni watu waliokuja hapa na kuianzisha hii kazi. Nao waliomba na wameamini ya kwamba Mungu angefanya mambo haya katika siku za mwisho, na wamewafundisha ya kwamba yangetukia, nayo haya hapa, yakitendeka sasa, moja kwa moja mbele ya macho yetu.

9 Sasa, tunawatakeni mkumbuke ya kwamba maombi ndiyo nguvu kuu kuliko zote zilizomo ulimwenguni, ni maombi. Maombi hata hubadilisha nia ya Mungu. Ni wangapi wanaojua hilo? Hiyo ni kweli. Mungu alimwambia nabii siku moja, panda ukamwambie mfalme, Hezekia, kasema, "Nenda kamwambie atengeneze mambo ya nyumba yake, maana atakufa."

10 Ndipo basi wakati nabii Isaya (Mngeweza tu kuwazia aibu ya nabii huyo?), wakati alipopanda juu kando, na maskini hao watu nje ya malango, "Loo, nabii mkuu, Neno la Bwana ni nini kwa mfalme wetu mwema?"

"BWANA ASEMA HIVI, atakufa."

Hapo walisimama askari langoni, "Loo, nabii mkuu, Neno la Bwana kutoka kwa mfalme wetu ni nini?

"BWANA ASEMA HIVI, atakufa."

11 Hezekia aliuliza hali yake: "Utakufa, hutatoka kwenye kitanda hiki." Naye alijua hilo lilikuwa ni Neno la Bwana, kwa hiyo akaelekeza uso wake ukutani na kulia kwa uchungu, na kusema, "Bwana, nakuomba unifikirie. Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu." Huo ni ushuhuda mkuu. "Nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu." Alitaka miaka kumi na mitano zaidi ya maisha.

12 Sasa, inaonekana kana kwamba kama Mungu alitaka kumjalia, yeye alikuwa ndiye mtu mkuu zaidi katika—katika hiyo milki, ilionekana kana kwamba Yeye angalisema tu, "Vema, Hezekia, mimi—Hezekia, nitakuacha uishi miaka kumi na mitano zaidi." Lakini mnaona, Mungu ana utaratibu, njia ya kufanya mambo. Badala yake, Mungu alishuka kwenye kichaka kidogo kwenye kichaka mahali fulani alipokuwa nabii Isaya, na kusema, "Rudi ukamwambie ya kwamba nilimsikia. Nitamjalia." Sasa, mnaona, maombi yalibadilisha mambo, mnaona, maombi yalibadilisha mambo.

Vema, aibu ya nabii huyo akirudi, "Kwa nini unarudi, nabii wa Bwana?"

"BWANA ASEMA HIVI, ataishi."

Hao askari, "Vipi kuhusu hilo?"

"BWANA ASEMA HIVI, ataishi."

13 Mnaona? Mnaona, ni kitu gani kilichosababisha hilo? Kutoka tu mautini kuingia uzimani, maombi yaliibadilisha, yakabadilisha hiyo hali kutoka mautini kuingia uzimani. Itakufanyia jambo lile lile. Itafanya jambo lile lile kwangu mimi. Ni mtazamo wetu kwa Mungu.

14 Na sasa kumbuka, ya kwamba kama umeomba lolote wala huamini moyoni mwako kwamba litatendeka, halitatendeka, haidhuru utaomba mara ngapi. Lakini unapoamini, hakuna kitu cha kulizuia lisitendeke. Ha—halina budi kutendeka. Lazima litendeke.

15 Nina umri wa miaka hamsini na miwili na nimekuwa katika huduma kwa, hii ni kama miaka thelathini na mmoja. Nami nimejua kuhusu kutukia kwa maono haya tangu nilipokuwa bado si zaidi ya miaka miwili, wakati lile ono la kwanza lilipokuja. Ninaamini ya kwamba karama na mwito havina majuto. Ninaamini ni—ni karama ambazo tumepewa na nia ya Mungu Mwenyewe.

16 Sasa, kuna karama tisa za kiroho zinazoingia katika kila shirika la mahali hapo, tunaamini hilo, Wakorintho wa Kwanza 12. Lakini kuna karama tano ambazo Mungu ameweka kwa ajili ya kanisa, karama za mwili. Ya kwanza ni gani? Mitume, na huyo si, kwa kweli, katika siku zetu, ni mmishenari, kwa sababu *mtume* na *mmishenari* ni neno lile lile. *Mmishenari* maana yake ni "mtu aliyetumwa." *Mtume* maana yake ni "mtu aliyetumwa." Mnaona? Mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti, mnaona, karama tano. Sasa, mtu hawezi kuwa mtume ati kwa sababu anataka kuwa. Mungu aliwaweka hao kanisani. Wala hawezi kuwa nabii ati kwa sababu anataka kuwa.

17 Sasa, kuna karama za unabii kanisani, lakini kuna tofauti kubwa kati ya karama ya unabii na nabii. Mnaona? Karama ya unabii haina budi kusimama mbele ya waamuzi watatu na kuchunguzwa kabla hata haijatolewa kwa kanisa, kama ni kweli. Huenda ikawa juu ya mwanamke *huyu* usiku wa leo, wala isije tena maishani mwake mwote, huenda ikawa juu ya mwanamke *huyu* kesho yake usiku, na mwanamume *yule* kesho yake usiku. Mnaona, ni—ni karama za mahali hapo katika mwili. Lakini unabii ni ofisi, nabii; hiyo ni tangu kuzaliwa, mnaona, inatokana na kuzaliwa.

18 Yeremia alikuwa ni nabii, Mungu alisema, "Kabla hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako, nalikujua, na kukutakasa, na nikakuweka kuwa nabii kwa mataifa." Yohana

Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, Isaya alimwona: "Sauti ya mtu aliaye nyikani," nabii wa Bwana. Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu tangu bustani ya Edeni, ule Uzao wa mwanamke ambao ulikuwa utakiponda kichwa cha nyoka.

19 Kama vile mzee Mbunge Upshaw alivyosema, "Huwezi kuwa chochote usicho." Mbunge wa Marekani, aliyegombea urais, yeye alijua vizuri zaidi, bali a—alitumia tu lugha yangu, njia yangu ya kulielezea. Lakini hiyo ni kweli. Unaweza tu kuwa . . . Na hiyo ndiyo shida yetu siku hizi, marafiki. Ulimwengu mzima unaonekana kuwa hivyo. Kama tungekuwa tu kile Mungu anachotufanya kuwa, kwamba, basi wewe ni—wewe ni—wewe ni, kuna, baragumu haitatoa sauti isiyojulikana basi, itatoa sauti inayojulikana, na ulimwengu wote utaijua, mnaona, wakati itakapopigwa sawa.

20 Na kwa hiyo, mhudumu hawezi kuwa mhudumu ati kwa sababu baba na mama yake wanamtaka awe mhudumu, hana budi kuitwa na Mungu apate kuwa mhudumu. Hakuna kitu kingeufanyia moyo wangu vizuri zaidi kuliko kujua kwamba mwanangu, Billy Paul, angekuwa mhudumu. Lakini kumpeleka shuleni na kumfanya mhudumu, afadhali angekuwa mtu wa kusafisha chombo cha kutemea mate kuliko kuwa hivyo, kitu asicho. Mnaona? Samahani kwa usemi huo mbaya. Sikupaswa kusema hivyo. Unaona? Hausikiki sawa hapa, bali mnajua ninalomaanisha. Afadhali angekuwa kitu kingine.

21 Lakini Mungu amemtumia Billy. Amekuwa msaidizi wangu muhimu, mwanangu. Kwa sababu wakati tulipoanza kutoa kadi za maombi kwa mara ya kwanza, tuligundua kwamba, kulikuwa na mtu mmoja mle ndani, wa kwanza alikuwa ni mhudumu, tulikuwa na wakati mgumu sana kuhusu kadi za maombi, kwanza, tungezituma kila mahali, ambapo tulikuwa tunaenda kuwa na mkutano, wachungaji wote wanaodhamini wangepata kadi mia moja kwa ajili ya kusanyiko lao. Mchungaji wa kwanza alipoliingiza kundi lake ndani, hilo karibu lilitosha, hao wengine hawakufika hapo.

22 Kwa hiyo basi tukaanza, kasema, "Vema, tutashuka twende siku ya kwanza tutakayokuja na kusambaza kadi zote za maombi." Na sasa, hiyo si kwa ajili ya mikutano midogo ya kanisa, hiyo ni kwa ajili ya kumbi kubwa. Na kwa hiyo, vema, siku ya kwanza ingetubidi kusambaza kadhaa, kadi mia tatu za maombi. Haikumfaa mtu yeyote kuchelewa kuja, maana hakika hawakuingia kwenye mstari wa maombi, maana hatungeweza kuzichukua zote. Nne, tano, ama sita kila usiku zilifanya yote tuliyoweza kufanya. Mnaona?

23 Na, halafu, nyingine tuliyokuwa nayo, tulikuwa na mhudumu wa kusambaza kadi za maombi. Vema, tukagundua wakati alipoingia mjini, na dhehebu lake mwenyewe, ilimbidi

kuwaonyesha upendeleo kidogo la sivyo wangemtenga, kwa hiyo, ama kusababisha manung'uniko.

24 Ndipo nikamwingiza mtu wa kawaida tu, na nikamwona akijaribu kuuza kadi ya maombi. "Nihakikishie," mtu fulani akasema, "kama utanihakikishia mke wangu atakuwa kwenye safu ya mbele, nitakupa dola mia tano." Ndipo mtu fulani akalisikia, ndipo a—akaliingilia kabla halijatukia.

25 Kwa hiyo basi hilo lilikomesha hilo. Ndipo nikamchukua ndugu yangu, nilijua asingeuza kadi ya maombi. Na hilo ndilo ulimwengu ungekuwa ukitafuta, mwajua, kitu kama hicho.

26 Lakini mtu yeyote anayejua hii mikutano, pesa zimekuwa ndicho kitu cha mwisho katika mikutano yetu. Nimejaribu kudumisha jina zuri safi. Kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu, nimekuwa nikihubiri miaka thelathini na mmoja, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu, wala kamwe sikuomba moja, kamwe sikusudii kuomba, hilo silo, hatuji kwa sababu ya pesa, tunakuja kuona yale mema tunayoweza kufanya, kujaribu kuungana pamoja na hawa ndugu hapa kusaidia kuvuta mzigo, hiyo ndiyo kazi yake.

27 Karama hizi zi—zingeweza kunifanya milionea katika si—siku chache. Mnajua ni kitu gani. Naam, nadhani mlisoma kwenye gazeti ambapo yule mwenye milioni nyingi huko California alinitumia milioni moja na laki tano katika toleo moja. Mawakala wa FBI walizileta kwenye—walizileta kwenye...nikasema, "Nakataa hata kuziangalia." Mnaona? Nikasema, "Sichukui pesa." Nisingeweza kuchukua pesa, vitu kama hivyo. Loo, rehema. Ati mimi? Sina, sina nguvu za kiakili za kushughulikia kiasi hicho cha pesa. Kwa hiyo basi, vipi kama ingekuwa hivyo? Sina budi kuzihofia. Mnaona? Acheni wazihofie. Nikizihitaji, Bwana atasema, "Mpeni *kiasi fulani*," Mnaona? Kwa hiyo basi, hilo ni sawa. Uh-huh.

28 Sininii...Nilikuwa nikizungumza, Ndugu Roberts, Oral Roberts, yule shujaa mkuu mashuhuri, Ndugu Roberts. Mtu huyo hana budi kuwa na karibu dola elfu kumi kwa siku. Whiu! Vema, Mungu alijua alichokuwa akifanya wakati hakuweka jukumu *hilo* juu yangu. Hakika nisingeweza kufanya hivyo. Dola elfu kumi kwa siku, hizo zingenitia wazimu kupokea elfu kumi kwa siku.

29 Na hayo mengine...Vema, sasa, vipi kama ilinibidi kuwa na elfu kumi kwa siku, naye Bwana aliniita, nije huku Grande Prairie, ningefanya nini juu yake? Mnaona? Si—sina vipindi vyovyote vya redio, sina chochote cha kuuza, wala si lazima niwe na senti kumi kwa siku. Mnaona?

30 Jambo pekee ninalopaswa kufanya ni kujiweka huru na mambo yote, ili niweze kwenda popote Yeye anaponiambia. Kama ni huko chini...Nilifanya uamsho wa siku mbili usiku mahali ambapo palikuwa na watu thelathini. Najua ilikuwa ni

duni. Ilikuwa karibu kumi chini ya sufuri, nao wanasimama tu huko nje wakiganda, pamoja na watoto wachanga wagonjwa na kadhalika. Lakini Bwana aliniambia niende, kwa hiyo ni—nikaenda tu.

31 Ndipo basi kama Yeye ananitaka, niende Afrika kuwahubiria laki moja, laki mbili, Yeye huliweka moyoni mwa mtu fulani kunitumia hundi nipate kwenda huko, kwa hiyo ninaenda tu huko. Kwa hiyo, mnaona, Baba Yangu anamiliki yote, wala sina haja ya kuhofia juu yake. Ninii tu, ninapenda kuwa hivyo, ambapo ninaweza tu kwenda popote Yeye anaponiambia niende. Mnaona?

32 Jamani, Chris, tusingeweza kwenda kuwinda kama ingenibidi kuwa na dola elfu kumi kila siku. Kamwe nisingeweza kufanya hivyo. Lakini nina furaha kuwa tu huru, ili niweze kuja kwa ndugu zangu, maskini yule ndugu, aliye na kanisa dogo sana, ama popote Bwana aongozapo, nenda tu aongozapo. Hivyo ndivyo ninavyopenda kuwa: huru, mnaona, hakuna kitu cha kunifunga wala kunishikilia, na tayari kwenda popote, wakati wowote, lolote Yeye asemalo nifanye. Nami nimeona ni maisha mazuri, mazuri sana.

33 Nami ninaninii, ninaweza kusema hili kwa uaminifu kutoka kwenye mimbara hii, ambao huenda ukawa ndio ujumbe wa mwisho nitakaopata kuiletea jamii ya binadamu, mnaona, nina umri wa miaka hamsini na miwili, hivi majuzi, na kamwe maishani mwangu sijawahi kumwomba Mungu jambo lolote kwa uaminifu, ila ambalo Yeye alinipa, ama kuniambia ni kwa nini asingeweza kunipa. Sasa, hiyo ni kweli. Mara nyingi nimeombea mambo, Yeye amenikataza, bali angeniambia ni kwa nini, na ni ninii, daima, njia Yake ndiyo bora zaidi. Nami nikagundua kama angelinipa, mimi, i—ingeniangamiza. Mnaona? Kwa hiyo ninaendelea mbele tu, nasema, "Bwana, chochote unachotaka niwe nacho, mimi hapa." Na kwa hiyo Yeye daima hunishughulikia.

34 Lakini angalieni mikutanoni, wakati wowote mnaposikia, wakati upambanuzi unapoendelea, Yeye anakwambia, unafanya hivyo mwenyewe, hujui, bali ni roho yako mwenyewe, kama yule mwanamke akigusa vazi Lake. Lakini wakati anapojibu, hilo ndilo unalovuta, wewe mwenyewe, kutoka kwa Mungu. Mnaona, Mungu hakuwa akitumia karama Yake.

35 Sisi sote tunajua ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Sasa, tunajua ya kwamba Kristo, Yesu, Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Lakini kwetu sisi, tunaye Roho kwa kipimo, tuliyepewa kila mmoja kwa kufaidiana.

36 Sasa lakini, tuseme, kwa mfano, kama nilienda hapa nje baharini na kuchota kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, usingeweza kuyakosa. Unaona? Lakini ningeweza kupeleka

hicho kijiko cha maji kwenye maabara, nayo yana kemikali zile zile ndani yake ambazo bahari nzima inazo, ni kwamba tu si kiasi hicho.

37 Vema, basi, tunapowazia juu ya Roho wa Kristo tuliye naye ndani yetu, mnaona, ni kijiko kimoja tu cha yale yaliyokuwa ndani Yake. Mnaona? Alikuwa na yote ndani Yake. Yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamwaga ndani ya Kristo; yote aliyokuwa Kristo, aliyamwaga ndani ya Kanisa.

38 Ni Wapentekoste wangapi waliopo hapa? Hebu tuone mkono wenu, enyi Wapentekoste. Vema. Mnajua kile Mungu alichofanya kwenye Siku ya Pentekoste? Biblia ilisema walikuwa wamekusanyika na kuomba katika chumba cha juu, na kwa ghafla kukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, nao ukajaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Ndipo zikawatokea Ndimi zilizogawanyika, kama za moto, zikamkalia kila mmoja wao, na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kunena.

39 Sasa, tunajua ya kwamba Mungu alikuwa ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli kupitia nyi—nyikani. Mungu alikuwa akifanya nini basi? Alikuwa akitenganisha, hizo Ndimi za Moto zilikuwa zikitengana, Nguzo hiyo kubwa ya Moto, na kujigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake.

40 Basi, ndugu, tunapaswa kuwa nini? Ndugu, jamani, pamoja tutasimama, tukigawanyika tutaanguka. Kwa hiyo ninii kuu . . . Kama kanisa kuu la Mungu, kama ibilisi anaweza kuingia ndani yao na kuwafanya waseme, “Mimi ni *hili*, nawe, kwa sababu wewe ni mfuasi wa *hili* kamwe hatuwezi kushirikiana pamoja,” haitambidi kufyatua risasi. Tunapigana sisi kwa sisi. Mnaona?

41 Lakini ukuta huo unapobomolewa, wala hatujagawanyika, sisi sote ni ndugu wamoja, mnaona, sote ni Roho mmoja katika Kristo, Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwetu pamoja, ili pamoja tuweze kuwa Kanisa kuu lililokombolewa la Mungu aliye hai, basi mtaona jambo fulani likitukia.

42 Sasa, ukiangalia, wakati Yeye anapokuzungumzia, kama akijibu, “Ni BWANA ASEMA HIVI, mambo *fulani* yatatukia,” sasa, wewe andika hilo. Huenda usiweze kuona to—tofauti yoyote papo hapo, huenda usiione kwa muda fulani, Mungu hufanya ahadi, lakini Yeye hutimiza ahadi Yake.

43 Naam, ninapenda kurejea kwenye hili. Wewe, hivi ulijua ya kwamba watu wengine hufikiri tu kwamba kwa sababu hilo halitukii mara moja, hiyo ni, hamna—hamna lingine, kwamba Mungu hakukusikia? Hilo ni kosa. Kama unaamini, lilitendeka, lakini kama hukuliamini, mbona, haileti tofa-. . . lisingetendeka kwa vyovyote vile. Lakini kama unaamini, ni bidhaa iliyokamilika papo hapo, u—unapoliamini.

44 Sasa, hapa kuna mambo mengi sana ningeweza kurejea. Wakati mmoja kulikuwako na maskini wanawake kadhaa. Ninapenda kurejea jambo hilo, kwa sababu sikuzote lilidumu nami. Ilikuwa jukwaani. Kulikuwa na maskini mama mmoja aliyekuja jukwaani, na, maskini mke wa nyumbani, maskini mama, ndipo Roho Mtakatifu akamwambia, "Wewe ni *Fulani-wa-fulani*, wewe—wewe ni mwanamke *fulani-fulani*."

"Ndiyo, ndiyo."

"Nawe unaugua ugonjwa wa tumbo ambao ni, ulikuwa kwa daktari siku chache zilizopita, naye akakwambia, ulikuwa na kidonda cha tumbo."

"Naam, ndivyo ilivyo."

"Mume wako anafanya kazi kwenye *ninii*. . . "

"Naam, hiyo ni kweli," yote haya.

Ndipo akaanza kwenda, kisha Roho akanena "BWANA ASEMA HIVI, umeponywa."

Loo, jamani, hilo halina budi kutukia. Hilo halina budi kutukia.

45 Ndipo akaenda nyumbani, naye akasema, "Vema, nimepona. Mume wangu, kabla sijafika huko, ninakutaka, uninunulie sambusa." Karibu imwue. Siku kadhaa baadaye alikuwa angali ananinii, angekuwa mgonjwa sana wakati akila.

Ndipo mumewe hatimaye akasema, "Unaaibisha huduma." Kasema, "Hupaswi kushuhudia jambo hilo."

46 Majuma mawili yakapita. Alikuwa angali anajaribu kula. Mgonjwa tu vilevile, kama wakati angekila. Nanii. . .Kwa hiyo mumewe akamwendea daktari, akamwambia. Kasema, "Utamwua."

47 Kasema. . .lakini akasema, "Tazama, mtu huyo hakunijua, na kama Roho alikuwa amesimama pale, ama pamoja naye, ambaye angeweza kumwambia mimi ni nani na shida yangu ilikuwa nini, ninaamini ilikuwa ni Roho wa Mungu." Basi akasema, "Niishi nife, yeye alisema 'BWANA ASEMA HIVI.'" Kasema, "Ninaliamini." Hiyo ni kweli. "Ninaliamini."

48 Asubuhi kadhaa baadaye, ambazo zilikuwa yapata majuma manne hivi baada ya yeye kuombewa. . .Mnaona, hilo halikumaanisha yeye hakuwa ameponywa, aliponywa papo hapo. Ibrahimu alipewa ahadi ya kwamba angempokea mwana, na miaka ishirini na mitano baadaye kabla hajampata, lakini alikuwa na imani thabiti, akimtukuza Mungu. Hivyo ndivyo Wapentekoste halisi wanavyopaswa kuwa, Uzao wa Ibrahimu.

49 Kwa hiyo asubuhi moja, akasema. . .Vema, wakati huo ni—nilikuwa umbali wa maili mia tatu kutoka mahali hapo, katika mkutano mwingine wa uamsho, naye akaja mahali hapo kushuhudia. Akasema, "Mume alienda kazini asubuhi hiyo,"

akasema, “loo, tumbo langu lilikuwa linawaka moto,” naye akasema, “baada ya kitambo kidogo, nilikuwa nikiosha vyombo vyangu, nami nilikuwa nikilia,” akasema, “nikiwazia tu, ‘Ee Mungu, jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi ulivyo mkuu! Unalifanya jua liangaze, Wewe—Wewe unafanya mambo haya yote makuu.’” Kisha kasema, “Jinsi Wewe ulivyo mkuu, Ee Mungu,” namna hiyo, akilisifu tu Jina Lake, huku amesimama pale.

Akasema hisia ya ajabu sana ilipita juu yake. Naye akasema aliwazia, “Sijui hiyo ilikuwa ni nini?”

50 Unaona, sasa, haikubidi kuhisi chochote. Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Je, uliamini?” Mnaona? Amini.

51 Lakini basi akahisi kitu fulani kikipitia juu yake. Akasema, “Vema, sijui hiyo ilikuwa ni nini,” kasema, “hisia tu ya ajabu, najisikia vizuri sana,” akaendelea tu, kasema, “labda, nilikuwa tu nikimsifu Bwana, ni Roho Mtakatifu alinibariki.”

52 Akaendelea tu kuosha sahani, akaona njaa sana, kwa hiyo nadhani mama wote wako namna hii, watoto walikuwa wameacha shayiri kwenye sahani, kwa hiyo akashikwa na njaa sana, na hicho ndicho kitu ambacho kingemwasha sana, kilikuwa ni shayiri, kwa hiyo akachota tu kijiko kimoja, ama viwili, vya shayiri akala. Kwa hiyo baada ya kuimeza, aliwazia, “Vema, haiwezi kuchoma vibaya zaidi.” Lakini katika dakika chache, haikuwa ikichoma. Kwa hiyo akachota vijiko vingine vichache, haikumsumbua, kisha akachukua kipande cha tosti, hiyo haikumsumbua. Kwa hiyo akaenda tu na kujikaangia mayai yake mawili, akachukua tosti, na kikombe cha kahawa, naye akawa na yubile ya ulaji. Kwa hiyo akaninii tu—akaketi tu chini na kula kiamshakinywa kizuri. Akangojea kama saa moja na nusu, saa mbili, akajisikia tu mzima, akishikwa na njaa tena.

53 Kwa hiyo akajisikia vizuri sana, akakimbia kwa jirani. Naye jirani yake alikuwa mbele kidogo kwenye mstari wa maombi, usiku uliotangulia, naye alikuwa na uvimbe mkubwa mno shingoni mwake, ndipo jambo lile lile likatukia, aliambiwa yote kulihusu, kasema, “BWANA ASEMA HIVI, uvimbe huo utatoweka.” Na kwa hiyo alitaka kukimbia kwa jirani yake, milango michache chini barabarani, kile kilichotukia. Naye akasema alipofika kule alidhani walikuwa na ibada ya mazishi ama kitu fulani, makelele yote na mayowe, aliyopata kusikia. Akafungua mlango kwa ghafla, naye huyu hapa huyo mwanamke, amesimama ameshika shuka mkononi mwake, naye akasema, “Kuna nini, mpenzi?”

54 Akasema, “Unajua nini? Nilichelewa kuamka asubuhi ya leo,” kisha kasema, “Siwezi kupata kitu hicho mahali popote. Kimeondoka kooni mwangu. Nilitikisa kila shuka na kila kitu, siwezi kukipata popote.” Mnaona? Nao hawa hapa wote wawili, wakitoa ushuhuda.

55 Ilikuwa ni kitu gani? Wakati Mungu alipokwisha kutangaza kwamba Malaika alikuwa amepitia kwenye ujirani, akithibitisha Neno alilokuwa amenena katika Jina la Bwana. Mnaona? "Lijapokawia, hata hivyo litanena." Hiyo ni kweli, ndugu? Halina budi kunena. Kwa hiyo daima kumbukeni hilo.

56 Loo, ninyi ni wazuri sana hata ni vigumu kwangu kuliendea somo. Nina kitu niani mwangu ninachotaka kusema. Nitaninii tu, mtanivumilia kwa dakika chache tu za ziada, sivyo? Kwa hiyo tunatumaini kuingia kwenye mstari wa maombi baada ya kitambo kidogo.

57 Kwa hiyo tulipoenda Afrika hivi majuzi tu, kuwaonyesha . . . Sasa, ninamshukuru Mungu kwa ajili ya shule, kwa ajili ya makanisa, na kwa yote ambayo amefanya, ninamshukuru Mungu sana. Lakini hata hivyo, hivi mlijua agizo halikuwa hilo? Agizo la jumla lilikuwa, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Sasa, ili kuihubiri Injili, Injili ilikuja si kwa Neno tu, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.

58 Sasa, kama ukiendelea kulifuatilia, ninanukuu Marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kufundisha tu Neno hakutafanya hivyo. Lazima iwe ni Roho Mtakatifu akilidhihirisha Neno. Mnaona?

59 Lakini tulifanya nini? Tulienda, na kujenga shule, na madhehebu, na makanisa, na—na hospitali, ambalo ni sawa kabisa. Hatuwezi kusema jambo moja dhidi yao. Bali wazo halikuwa hilo.

60 Sasa, nilipoenda Afrika, ninakumbuka . . . Sasa, ndugu zangu wa Kibaptisti hapa, tafadhalini msininii . . . Mimi, ninakupenda, wewe ni ndugu yangu, mnaona. Lakini nilikuwa mhudumu wa Baptisti ya Kimishenari kwa miaka mingi, na wakati ningewaambia kuhusu mambo haya, wangenitishia sana, walisema ilikuwa ni ya ibilisi, na, loo, sikutaka uhusiano wowote na ibilisi, maana ninampenda Bwana Yesu. Wala kamwe sikujua neno juu yake mpaka aliponitokea na kuniambia ilikuwa ni kitu gani.

61 Sasa, niliporudi na kumwambia Dk. Davis, mwangalizi mkuu, nami nikasema, "Dk. Davis, nilikutana na yule ambaye huzungumza nami, na ilikuwa ni Mtu, naye akaniambia mambo haya, naye akaniambia nitahubiri kote ulimwenguni, na mambo haya yatatukia."

Akasema, "Ukiwa na elimu ya darasa la saba, nadhani, Billy, utawahubiria wafalme na wata- . . . "

Nikasema, "Hivyo ndivyo alivyosema, Ndugu.

Akasema, "Billy, ulikula nini usiku huo kwa ajili ya chakula cha jioni?"

62 Nikasema, "Vema, sasa, Dk. Davis, kama ndivyo ilivyo, afadhali hata nikupe kadi yangu ya ushirika sasa hivi,"

nikasema, "kwa sababu kwangu mimi ilikuwa ni Mungu, sijui ilikuwa ni nini kwako." Unaona? Na bila shaka mmesikia jambo hilo katika *Sauti ya Uponyaji*, yeye mwenyewe anahubiri uponyaji wa Kiungu sasa.

63 Kwa hiyo hata hivyo, wakati Malaika aliposema kwamba . . . Nami, nilipoingia Afrika, na kukuta, huko Afrika, niliona nini? Sidhalilishi chochote, ninashukuru sana kwa kila kitu ambacho Bwana amefanya, ninyi nyote kumbukeni hilo, kila kitu ambacho Bwana amefanya, ninashukuru. Lakini ninajaribu kusema tunaishi katika siku nyingine, kubwa kuliko hiyo sasa. Mnaona? Tuna—tunafikia mahali ambapo Mungu anataka kufanya mambo makuu kuliko yale ambayo amefanya. Anataka kulibariki Kanisa Lake.

64 Anatutaka tuje pamoja, na si kubishana kuhusu, "Mimi ni Assemblies of God," au, "Mimi ni Church of God." Inaleta tofauti gani? Sisi ni wa Kristo. Jambo ndilo hilo. Mnaona? Sisi ni wa Kristo. Si. . .hatupaswi kuwazia hilo. Na mmoja wetu akiendesha ngamia wenye nundu moja, ngamia wenye nundu mbili, na ngamia wenye nundu tatu. Inaleta tofauti gani?

65 Yakobo alichimba kisima kimoja, nao Wafilisti wakamfukuza kutoka humo, naye akakiita "Kijicho." Akachimba kisima kingine, nao Wafilisti wakamfukuza kutoka humo, naye akakiita "Ugomvi." Akachimba kisima kingine, kwa hiyo akasema, "Kuna nafasi kwa ajili yetu sote." Kwa hiyo nafikiri hivyo ndivyo ilivyo. Wale walio juu ya ngamia *wa kila namna*, tunaweza kupanda moja kwa moja na kupata maji ya kunywa. Kuna nafasi kwenye chemchemi kwa ajili yetu sote. Naam.

66 Kwa hiyo nilipofika kule, nilifikiri ningekuta, labda, wamishenari, kina David Livingstone kwenye kila kona. Lakini niliona nini ila, jamani, wamishenari walikuwa tofauti na vile nilivyodhani ilikuwa. Walikuwa na kiwanja huko nje, ambapo mtu mweusi ambaye asingeweza kudumisha rangi ya kujipaka ya kabila tena . . .

67 Wangeweza kuja hapa na kutufundisha maadili, hao watu wangeweza, katika Afrika. Hakika, wangeweza. Kwa mfano, katika kabila moja huko katika Basuto, kama Shangaan, Basuto, Xhosa, loo jamani, makabila mengi mbalimbali, lakini kama msichana, kamwe hawajui wana umri gani, lakini kama msichana si ninii, mwanamume fulani amemchukua, wao wana ndoa za kuoa wake wengi, lakini kama mwanamume fulani hajamchukua kama mke katika ukubwa fulani, hana budi kuondoa rangi yake ya kikabila na kuliacha hi—hilo kabila, kwa sababu kuna kasoro.

68 Kama ameninii, kabla hajaolewa, ama kuchukuliwa kuwa mke, anachunguzwa ubikira wake, kama akipatikana na hatia, hana budi kusema mtu ambaye amefanya hivyo, wote wawili

wanauawa pamoja. Kungekuwa na vifo vingi, kote Marekani kwa vyovyote vile, kama wangewachunguza namna hiyo. Lakini hakuna maisha ya usiku miongoni mwao. La, bwana. Wao ni safi, waadilifu, wawezavyo kuwa.

69 Na, basi, walikuja kwa makumi ya maelfu mkutanoni tulipokusanyika Durban. Nami nilikuwa . . . Billy alikuwa pamoja nami, nikasema, “Mwanangu, shuka uende ukasambaze kadi za maombi alasiri ya leo.”

70 Ndipo wakati aliporudi katika dakika chache, yeye pamoja na meya wa jiji, Sidney Smith, hawakuwa, hakuwa na mifuko kwenye koti lake. Akasema, “Kusambaza kadi za maombi? Hebu shuka uende kule ukajaribu mara moja!” Akasema, “Huwezi kufanya hivyo, Baba.”

Kwa hiyo nikasema, “Vema, sawa.”

71 Kwa hiyo, Bw. Smith, Sidney Smith, meya wa Durban, alinitoa nje, kasema, “Ndugu Branham, katika historia yote ya Afrika, hakuna kitu kama hiki kilichowahi kuonekana.” Naye akasema, “Ukumbi huo wa mbio za farasi wa Durban umejaa watu *sana*, mpaka wako kote kote ng’ambo ya pili. Maelfu mara maelfu, zaidi ya laki moja, wamelala tu pale,” kasema, “wanakuja kutoka, wanamiminika kutoka sehemu zote za nchi, nao waliwaleta wapendwa wao, majuma kadhaa kwa wakati, waliwaleta kupitia misituni, kufikia mahali ilipowabidi kuninii, simba angewafuata, ingewabidi kupanda haraka juu ya mti.”

72 Samahani kwa tamshi hilo, hilo ni . . . Mimi—mimi—mimi najua ninyi nyote mna Kiingereza bora kuliko changu, tulicho nacho kule chini.

73 Na kwa hiyo, ni—nina maskini Mjojia hapa, ninamtaka awazungumzie moja ya siku hizi usiku. Nena kuhusu kuwa na karama ya kufasiri! Yeye . . . Mtaninii, ninyi Yankee hapa juu kweli itawabidi kuwa nayo kuwasikia hawa Wajojia wakizungumza. Walikuja kwenye kituo cha mafuta, wakaomba moteli, nao walitaka kujua kama wanataka, yeye . . . wote, walisema alitaka tairi kuu kuu. Kwa hiyo, Georgia.

74 Kwa hiyo, hata hivyo, nasi tukatoka, tukaanza kwenda mahali hapa pazuri sana tulipokuwa tukienda, nasi tulipofika huko nje, tukitoka, tuliwaona hawa wenyeji mjini, wenyeji waliovaa blanketi, sasa, nao walikuwa na kibandiko kidogo shingoni mwao. Ndipo nikamwambia Sidney Smith, nikasema, “Meya, hivyo vibandiko ni vya nini?”

Akasema, “Loo, ni Wakristo.”

Nikasema, “Vema, kwa nini wanabeba sanamu?”

Akasema, “Waulize,” akasema, “Mtu yule,” kasema “yeye ni Mshangaani, ninaweza kuzungumza lugha yake, mwendee, mwite chochote utakacho.”

75 Kwa hiyo mimi, tukajongeza gari karibu naye, nami nikamwita Thomas, kwa sababu niliwazia hilo lingekuwa ni jina zuri kwake, mwajua, anadhaniwa kuwa ni Mkristo, huku amebeba sanamu. Nami nikasema, “Thomas.”

“Naam.”

“Wewe ni Mkristo?”

“Naam, naam, ndiyo,” yeye ni Mkristo.

Nikasema, “Kwa nini unabeba hiyo sanamu?”

76 Loo, baba yake aliibeba. Mnaona? Hiyo ni sababu nzuri. Siku moja simba alimfukuza baba yake, kwa hiyo a—akaiweka chini ile sanamu ndogo, na—na kuwasha moto, kisha akaomba ombi aliloambiwa na mchawi, yule simba akatoroka. Kwa hiyo ilikuwa ni mungu.

77 “Loo,” nikasema, “Mimi ni jagter.” *Jagter* maana yake ni “mwindaji.” *Leeu* maana yake ni “simba.” *Leeujagter*. Nikasema, “Moto ulimtorosha huyo simba, sio maombi ya mchawi.”

78 “Loo, vema, kama Amoyah,” *Amoyah* linamaanisha ‘upepo,’ nguvu zisizoonekana kama vile Mungu, ambazo huzioni, wajua, kama vile Roho Mtakatifu, “kama akishindwa, huyu asingeshindwa.”

Kwa hiyo akaibeba tu kwa ajili ya usalama. Hizo ndizo nguvu za Ukristo.

Sidney Smith akasema, “Unaona?” Kasema, “Unaona ni kwa nini ni vigumu kuingia hapa kama mmishenari?”

Nikasema, “Naam, bwana.” Tukaenda mkutanoni.

79 Kwa hiyo alasiri hiyo, huko mbali ng’ambo ya huo uwanja nilikuwa nimechukua. . .Ilinibidi—ilinibidi kutumia wakalimani kumi na watano mbalimbali. Mnaona? Ungesema neno moja, halafu, useme, “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikuja duniani kuwaokoa wenye dhambi,” vema, ningeenda nikanywe maji, na kuketi chini, nizungumze na mtu fulani, wakati likipitia kwa hao wakalimani wote, inakubidi kuandika yale uliyosema upate kujua mahali pa kurudia. Kwa hiyo ningewapa ujumbe mdogo rahisi wa Biblia, kile Yesu alichokuwa.

80 Nami nikasema, “Kila mmoja wenu wamishenari nendeni mkawachukue watu watatu kutoka katika makabila fulani huko nje mwapandishe huku.” Kulikuwako na Waislamu kama elfu kumi pale pia, ambao walikuwa ni Wahindi. Na sasa, si Mhindi wetu wa Marekani, bali Mhindi, kutoka India. Kwa hiyo nikasema. . .

81 Wao ni wagumu sana, sana. Nilimwona mmishenari mmoja pale, akasema, “Loo, Ndugu Branham, nimekuwa hapa miaka ishirini, nikapata kito kimoja cha thamani.” Mnaona, Wa—

Wa—Waislamu walitoka kwenye jamii ya kale ya Wamedi na Waajemi, nao hawabadiliki wala kubadilisha sheria zao, mwajua. Akiishakuwa Mwislamu, ndugu, huwabadilishi. Mnaona?

82 Kwa hiyo wakati likiendelea, hivyo basi wakawaita... Nikasema, "Chukueni watatu kutoka katika kila moja ya hayo makabila muwalete." Kwa hiyo wakashuka kule, na hatimaye wakawaleta huku. Basi ikawa wa kwanza jukwaani alikuwa ni mwanamke wa Kiislamu, alama nyekundu katikati ya macho yake. Naye alikuwa ni Mwislamu ukoo safi.

Nami nikasema, "Je, unaelewa Kiingereza?"

Akasema, "Naam, bwana."

Nami nikasema, "Vema, wewe ni Mwislamu?"

Akasema, "Naam." Nafikiri mnalitamka hapa *Mwislamu*. Lakini, akasema, "Naam."

Nami nikasema, "Basi kwa nini ukaja kwangu nami ni Mkristo? Kwa nini hukuenda kwa kuhani wako?"

Akasema, "Ninaamini ya kwamba unaweza kunisaidia."

"Loo," nikasema, "kama Mwislamu, hupaswi kuamini hilo. Unapaswa kuamini ya kwamba kama Mwislamu ni...kama nabii Muhammad ni mtumishi wa Mungu..."

83 Wanamwamini Mungu. Mnaona? Wao ni—wao ni watoto wa Ibrahimu, bali si wa ahadi, tunafahamu hilo. Mnaona? Kwa hiyo yeye...wao—wao hupiga adhana hiyo kubwa asubuhi na kusema, "Kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, na Muhammad ndiye nabii Wake."

84 Tunasema, "Kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, naye Yesu ni Mwanawe." Mnaona? Sasa, hiyo ndiyo tofauti. Naye Mwislamu anasema, "Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana, Roho kuwa na Mwana." Kwa hiyo wao, na kwa hiyo wao...

Nikasema, "Vema, kwa nini hukuenda kwa kuhani wako?"

Akasema, "Ninaamini ungeweza kunisaidia."

"Vema," nikasema, "Je, umewahi kusoma Agano Jipya?"

Akasema, "Naam."

"Umeutafakari Ukristo?"

Akasema, "Nimeutafakari."

Nikasema, "Kwa nini ukauchagua Uislamu?"

85 Akasema, "Vema, kwa sababu nafikiri ya kwamba—ya kwamba dini ya Kiislamu haikutoa ahadi zozote, bali Biblia ya Ukristo ilitoa ahadi, kupitia kwa Yesu Nabii, kwamba wanafunzi Wake wangefanya jambo lile lile alilofanya." Kisha akasema, "Mohammed hakutoa ahadi kama hiyo. Kwa hiyo, wote wawili waliahidi uzima baada ya mauti, wala sijaona hata mmoja wa

Nabii Yesu, wanafunzi Wake, akifanya yale aliyofanya, kwa hiyo mimi ni Mwislamu." Hilo ni jibu zuri sana, la busara. Mnaona?

Nami nikasema, "Vema, Yesu anatoa furaha tele."

Akasema, "Sasa, Uislamu unaweza kutoa saikolojia kadiri tu dini ya Kikristo inavyoweza."

86 Mhemuko mwingi vivyo hivyo, wanaweza kupiga makelele kwa sauti kubwa vivyo hivyo, wanaweza kupiga mayowe kwa nguvu vivyo hivyo tu, wanaweza kufanya mengi kama tufanyavyo sisi. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kama hujui unachozungumzia, afadhali usiwakaribie. Unaona? Achana nalo.

87 "Vema," nikasema, "basi umesoma Agano Jipya. Yesu, kama ulivyomwita, Nabii, nilimwita Mwana wa Mungu," nikasema, "kweli Yeye alikuwa ni Nabii. Wahusika wa Agano la Kale wanapaswa kuwaamini manabii wao, Naye alikuwa Mfalme Nabii, Mungu Nabii. Nao walikuwa wakimtazamia. Hivyo ndivyo tu nilivyouleta ujumbe wangu."

Akasema, "Kweli, bwana. Kwa hiyo niliomba niwe ndiye atakayekuja huku."

88 Nikasema, "Ni wangapi wenu ninyi Waislamu huko nje mnamjua mwanamke huyu?" Wengi wao. Nikasema, "Sasa, kama Yesu, Mwana wa Mungu, amenitia mafuta kwa Roho Wake, nami ninaweza kukwambia, basi, kama tu vile Yeye angefanya kama angekuwa amesimama hapa," nikasema, "kuhusu kukuponya, tayari amefanya hivyo, sifa zote za wokovu Wake alizotununulia pale Kalvari tayari zimekwisha, jambo pekee angaliweza kufanya lingekuwa ni kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Hiyo ni kweli. Aliahidi wanafunzi Wake wangefanya vivyo hivyo."

Kasema, "Ninaelewa."

89 Ndipo Roho Mtakatifu akaja. Nikamwambia yeye alikuwa ni nani kwa Roho Mtakatifu. Nikasema, "Sasa, mume wako ni mtu mfupi, mnene, mwenye masharubu, alikuwa kwa daktari hivi majuzi, na, pamoja na wewe, naye akakufanyia uchunguzi wa kike. Yeye alikwambia, ulikuwa na uvimbe kwenye ovari."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Vipi kuhusu hilo sasa?"

Akasema, "Ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu."

Alasiri hiyo karibu Waislamu elfu kumi walifanya jambo lile lile. Mnaona, mnaona, mnaona? Si theolojia, bali kuona nguvu za Mungu, mnaona, marafiki.

90 Aliyefuata alikuwa ni mwanamke mzungu, Mwafrikana. Nikamwambia kwamba alikuwa na nundu kwenye ziwa lake,

lakini ajiandae kwa ajili ya mauti, nilikuwa nimeona ibada ya mazishi yake. Wakamtoa hapo uwanjani, amekufa.

91 Usiku uo huo mwanamke mmoja aliyekuwa amekufa yapata saa nne, rafiki wa meya, alifufuliwa akawa hai tena. Msichana, akafa. Mnaona, kama ningeweza kuponya, *ningalimponya*. Nikasema, “Ninaweza tu kusema yale ninayoona.”

92 Aliyefuata alikuwa ni mvulana mdogo, mwenye makengeza aliyeingia mstarini, maskini Mzulu. Yeyote wenu ninyi ndugu wamishenari? Wazulu, Mitchel, unajua jinsi Wazulu walivyo, jamaa mkubwa mnene, wastani wa ratili mia tatu. Wanatupa assegai zao mwajua (Maskini Mshungai hana budi kuudhibiti wake.), Mzulu mkubwa. Ndipo walikuwa wamekula mlo huu, mwajua, damu hiyo na chochote cha kuiunganisha pamoja. Nayo macho yake madogo yalikuwa na makengeza yalivyoweza kuwa. Na huko Afrika, wao . . .

93 Ninyi akina dada mnapenda mayungiyungi? Loo, nafikiri yanapendeza. Wana baadhi yao yenye upana wa inchi kumi na sita, mayungiyungi makubwa mno ya kala jukwaani, baadhi yake manjano, na ni ya mwitu tu nyikani.

Kwa hiyo basi, wakati mvulana huyu mdogo, wakati alipokuja jukwaani, nilisema, “Sasa, mtu yeyote anaweza kuona kwamba macho yake yana makengeza.”

94 Kama wewe, je, ulikuwa Afrika wakati huo, Ndugu? Ulikuwepo? La, India. Loo, naam. Vema, mimi, labda nitapata nafasi ya kuzungumza juu ya India. Ulikuwa huko nilipokuwa India? Hukuwako. Huko ndiko nilikokuwa na kusanyiko langu kubwa kuliko yote, huko Bombay, laki tano kwa wakati mmoja. Kwa hiyo basi, huko ndiko nilikoona ninii, vema, siwezi kuingilia hayo, bali kulikuwa na . . . Amefanya mengi sana, nawaambia, ni ajabu sana.

95 Halafu, mvulana huyu mdogo akisimama pale, nami nikasema, “Mtu yeyote aliye karibu vya kutosha, anaweza kuona mtoto huyo ana makengeza.” Nikasema, “Nisingeweza kuyanyosha macho yake.” Nikasema, “Sina kitu cha kuyanyoshea macho yake, lakini,” nikasema, “labda huenda Roho Mtakatifu akanifunulia jambo fulani lililosababisha jambo hilo, halafu labda lingemfanya mvulana huyo mdogo ku— kuwa na imani ya kumwamini Kristo.” Nami nikamwambia, “Hebu niangalie.”

Naye mkalimani, mkalimani wa Kizulu, akasema, “Hebu niangalie.” Ndipo maskini jamaa huyo akaangalia juu.

96 Nikasema, “Alizaliwa hivyo.” Nikasema, “Sasa, mama na baba yake ni watu wembamba, si kawaida kwa Wazulu.” Nikasema, “Lakini anatoka katika nyumba ya Kikristo, kwa sababu katika kibanda chao kidogo kuna picha ya Kristo upande wa kulia wa ukuta unapoingia.”

Na yapata yadi mia moja huko nyuma, baba na mama wakainua mkono wao, huku wamesimama huko nje, "Umesema kweli."

97 Basi nilipomtazama mtoto huyo, macho yake yalikuwa yamenyoka kama yangu. Nikasema, "Hakika, mtu yeyote akiona jambo fulani limetendeka, macho yake, tayari yamenyoka. Pita, mwanangu." Nao wakampisha.

98 Na mara nikasikia fujo. Ni wangapi waliowahi kumjua Ndugu Bosworth? Maskini Ndugu Bosworth alikuwa mmoja wa rafiki yangu, F.F. Bosworth. Alikuwa amesimama pale, nami nikamsikia akibishania jambo fulani huko, fujo ya namna fulani. Basi ilikuwa ni daktari Mwingereza, naye alikuwa akibishana. Akasema, "Ninataka kuzungumza naye."

99 Ndugu Bosworth akasema, "Huwezi kufanya hivyo sasa, bwana," kasema, "ungesababisha tu ghasia." Iliwabidi kuwatenganisha. Walikuwa na vita vya kikabila, pia, mwajua. Na kwa hiyo, kasema, "Huwezi kufanya hivyo sasa," kasema, "wakati ndugu yetu akiwa chini ya upako huo, yeye huwaombea wagonjwa." Akasema, "Amini tu."

Kasema, "Ninataka kuzungumza naye."

Nikageuka, nikasema, "Kuna nini, Daktari?"

Akasema, "Ulijuaje mimi ni daktari?"

Nami nikasema, "Vema, unataka nini?"

Akasema, "Ninataka kukuuliza, Bw. Branham, ulimfanyia nini mvulana huyo?"

Nikasema, "Hakuna kitu."

Akasema, "Nilimweka jukwaani."

"Vema," nikasema, "hilo ni zuri sana."

100 Akasema, "Macho yake yamenyoka sasa, huyu hapa amesimama." Alikuwa ameweka mkono wake kichwani mwake, kasema, "Nilimweka jukwaani *pale*, macho yake yalikuwa na makengeza. Nimemwekea mikono yangu *hapa*, nayo macho yake yamenyoka." Kasema, "Sasa, Bw. Branham, ninaweza kuelewa telepathia yako," huko kuwazungumzia watu, na kuwaambia kuhusu shauku zao, na yale wamefanya, "lakini," kasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani, hivi ulimhiponozi mtoto huyo?"

101 Nikasema, "Madaktari wa Shirika la Madaktari la Uingereza walikupa leseni ya kufanya kazi ya udaktari, na hujui zaidi juu ya hiponozi kuliko hilo? Kama hiponozi itanyosha macho ya mtoto, hivi hufikiri ninyi madaktari mnapaswa kuanza kutumia uhiponozi, hiponozi?"

Akasema, "Bw. Branham, nataka ujue ya kwamba nimelelewa kumwamini Mungu."

Nikasema, “Hilo ni zuri sana, Daktari.” Ndipo wengine zaidi wakatokea. Nikasema, “Hebu kidogo. Achaneni naye.” Mnaona?

102 Naye akasema, “Vema,” kasema, “ninajua ya kwamba Mungu yuko katika yungiyungi lile. Halingeweza kukua, lina uhai tusioweza kuona, hatuwezi kuuona, chembechembe ya uhai. Tunajua ya kwamba Mungu yuko katika yungiyungi la sivyo lisingeweza kuishi.” Lakini kasema, “Niambie, Mungu huyo unayenena habari zake anaweza kuonekana *sana* hata angeweza kuyachukua macho ya mtoto huyo yenye makengeza na kuyanyosha, huku ukiwa umbali wa futi kumi kutoka kwake?”

“Vema,” nikasema, “Daktari, macho yake yamenyoka?”

Kasema, “Naam, bwana.”

“Vema,” nikasema, “Hivi nilimgusa?”

“La, bwana.” Akasema, “Basi hilo linamfanya Mungu kuwa mahali fulani kati ya *hapa* na *pale*, sivyo?”

Nikasema, “Kila mahali tu.” Na kwa hiyo basi mtu fulani akaanza kumvuta aondoke.

103 Akasema, “Hebu kidogo.” Ilikuwa ni maikrofoni kubwa ya utando, maana walikuwa, loo, labda yadi mia tano na bado kuna watu, mwajua, huko nje namna *hiyo*, hiyo maikrofoni kubwa. Akaenda kwenye hiyo maikrofoni, akasema, “Basi ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu.”

104 Ninataka kuwaambieni jambo fulani. Nilipokuwa nikiondoka Durban yapata majuma mawili baada ya hapo, kulikuwako na yapata watu ishirini ama thelathini elfu pale, wakitupungia mikono ya kwaheri na kila kitu, mwajua, “Rudini, rudini.” Ilichukua vichwa-. . .kurasa mbili na tatu za gazeti kila siku, hiyo mikutano, yale Bwana wetu aliyofanya.

105 Na hapo, katika jambo hilo, mnajua alichofanya? Alikimbia kwenye ngazi, akaruka kutoka kwa walinzi, na kukimbia huko nje na kunikumbatia kwa mikono yake, namna *hiyo*, akanikumbatia, kisha akaanza kunena kwa lugha. Naye akasema, “Ndugu Branham, mimi ni Mkristo. Ninarudi hudumani kuwa mmishenari,” daktari huyo Mwingereza. Na hiyo ikakamilisha siku hiyo.

106 Aliyefuata alikuwa ni mvulana aliyekuwa ameumbuka *sana* (Samahani, dada zangu, kama nikifanya kosa baya, uh, nikifanya kosa, hasa, nikisema jambo fulani ambalo sipaswi kusema, lakini hawavai, hawavai nguo, mnaona, wako uchi tu kama walivyokuja duniani.), ndipo wakati huyo mvulana alipokuja jukwaani, jamaa mdogo, alitembea kwa mikono yake, namna *hii*. Naye alikuwa amepinda kabisa, katika hali mbaya sana, nao walikuwa wamemfungia mnyororo shingoni mwake.

107 Nami nikasema, “Mwangalie maskini mwanadamu huyo. Kama mtu yeyote angeweza kumsaidia mvulana huyo wala

asimsaidie, mbona, angekuwa ni mnafiki." Nikasema, "Kama ningalikuwa na kitu chochote ningeweza kumponya maskini jamaa huyo, bila shaka ningemponya, bali siwezi kufanya hivyo, mnajua hilo, lakini," nikasema, "labda Roho Mtakatifu angeweza kunifunulia kitu ambacho kinaweza kumfanya aamini ya kwamba Mungu angemponya." Na kwa hiyo nikageuka kuangalia, nami, nilipokuwa nikimtazama, lile ono, siwezi kuelezea hilo, huwezi kumwelezea Mungu, hakuna haja ya kujaribu. Kama ungejaribu, haingekuwa [sauti ya Ndugu Branham ilialika—Mh.] (Samahani.), isingekuwa kwa imani tena.

108 Kwa hiyo mvulana huyo alikuwa pale, alionekana kuwa, loo, ningekisia alikuwa kwenye umri wa miaka ishirini na kitu, ishirini na miwili, ishirini na mitano, mahali fulani namna hiyo. Nami nikasema, "Sasa, nimeuvutia usikivu wake." Na sasa, kumbukeni, alikuwa akitembea kwa miguu yake, sehemu za nyuma zikitokeza juu namna *hii*, huku akiyumbayumba nyuma kama farasi, mwajua, farasi anayeyumbayumba, na kutembea kwa mikono yake, namna *hiyo*. Naye anafikiri nilimtaka a—acheze dansi ya kikabila. Wa—watu wanaoyaacha hayo makabila, wanaingia, nao wanawafanyia watalii vitimbi kwa kucheza dansi za kikabila. Alikuwa akisema "Uh, ba, ba, ba, ba."

109 Nami ni—nikasema, "Laiti ningepata usikivu wake kwa dakika moja, niishike roho yake." Naye akasema . . . Nikasema, "Loo, kile anachowazia sasa, kwa kweli hajiwazii mwenyewe." Nikasema, "Mvulana huyu alifanyika hivyo alipokuwa mtoto tu."

Papo hapo baba na mama yake wakasimama, *huku* chini kabisa, kwamba ni kweli. Mnaona?

Nikasema, "Yeye pia ametoka kwenye nyumba ya Kikristo, inayokiri kuwa ya Kikristo." Hiyo ilikuwa ni kweli.

110 Nikasema, "Lakini kile anachowazia ni ndugu yake," nami nikasema, "ndugu yake ama alikuwa amepanda mbuzi wa manjano ama mbwa wa manjano, naye akaanguka na kuuumiza mguu wake. Ametembea kwa fimbo mbili sasa kwa miaka mitatu au minne iliyopita." Lakini mimi . . . ndipo nilipoangalia nyuma, nikamwona ndugu yake akienda, akikimbia, akirukaruka, namna *hiyo*, nikasema, nikaangalia, nikasema, "Lakini, BWANA ASEMA HIVI, ndugu yake ameponywa." Naye akaendelea, namna *hii*.

111 Na huko chini kabisa, loo, karibu majengo mawili ya mji, nikasikia mlio mkubwa. Nao walikuwa na, nadhani, askari mia tatu, wanamgambo, mwajua, kidogo kudumumisha utaratibu. Naye huyu hapa ndugu yake anakuja na vijiti hivi juu ya kichwa chake, akiruka kwa nguvu tu alivyoweza.

112 Vema, ilichukua kama dakika ishirini, kuwatuliza tena, mnaona, kuwatuliza. Nikamtazama tena, nikasema, "Sasa, si—siwezi kufanya lolote ila kumwombea huyu mvulana." Ndipo nikaona kitu kama kivuli cha samawati juu yake, nami nikaangalia, na katika hilo ono huyu hapa amesimama, amesimama kwa miguu yake. Loo, ndugu, kuna, pepo wote kutoka kuzimu wasingeweza kuukomesha wakati huo.

113 Kama Yeye angeniambia ya kwamba—ya kwamba George Washington angefufuka kutoka kwenye makaburi ya rais, ningealika ulimwengu uje utazame likitendeka. Hiyo ni kweli. Yeye ni. . .Nimeona maelfu mara maelfu ya maono, nami nitamkumbusha mtu yeyote: hakuna hata moja lililoshindwa. Haliwezi kushindwa, ni Mungu, Mungu anawezaje kushindwa?

114 Kwa hiyo nilijua huyo mvulana ataponywa, nami nikawazia, "Hii hapa nafasi yangu, sasa hivi." Nikasema, "Ni wangapi hapa watampokea Kristo kama Mwokozi wao kama mvulana huyu ataponywa?" Kadiri tu nilivyoweza kuona, mikono hiyo myeusi: Washangaani, Basuto, kila mahali, namna *hiyo*, Wahindi, kila mahali.

115 Nami nikasema, "Simama kwa miguu yako, mwanangu, Yesu Kristo anakuponya." Bila shaka yeye, mkalimani, alimwambia hivyo, lakini huyo mvulana hata hakuwa na akili timamu. Kwa hiyo aliendelea tu kufanya "Uh, ba, ba, bla, bla," nami. . . akijaribu kucheza dansi, alidhani tulikuwa tukimleta kule kufanya vitimbi, mnaona, kucheza dansi. Kwa hiyo nikaenda pale na kuushika mnyororo waliokuwa wamemfungia, ambapo walimwongoza, Nikasema, "Simama kwa miguu yako, Yesu Kristo anakuponya." Ndipo huyo mvulana akasimama.

116 Basi aliposimama, machozi yalitiririka kwenye tumbo lake jeusi, akasimama pale, na kuangalia kote namna *hiyo*, kwa mara ya kwanza maishani mwake. Umati huo ukaingia tu *kichaa*. Huyo hapo, si kwamba tu aliponywa, akanyoshwa, bali akiwa na akili zake timamu. Mnaona?

117 Nikasema, "Ni wangapi wenu watampokea Yesu Kristo sasa kama Mwokozi wao binafsi, Yule anayewapenda?" Kisha nikasema, "Simameni kwa miguu yenu." Wenyeji elfu thelathini wanaovaa mablanketi wakasimama kwa wakati mmoja.

118 Ninyi Wakanada mnamjua Ern Baxter, sivyo? Ndugu Ern Baxter? Alikuwa amesimama pale pale jukwaani. Basi Ndugu Baxter akasema, "Ndugu Branham, ninaamini walimaanisha uponyaji wa kimwili."

Nikasema, "Hebu nilipitishe kwenye. . ."

Naye mzee Ndugu Bosworth huku analia tu. Akasema, "Ndugu Branham," akasema, "Roho Mtakatifu hivi sasa anauondoa uhai wangu kutoka kwangu."

119 Nami nikasema, “Sikumaanisha uponyaji wa kimwili, nilimaanisha kumpokea Kristo kama Mwokozi. Ninyi mnaobeba sanamu, kama mnaelewa, zivunjeni sanamu zenu ardhini.” Na kama dhoruba ya mavumbi, ambapo hizo sanamu zilivunjiwa. Wenyeji elfu thelathini wasio na ujuzi, waliovaa blanketi wakamjia Kristo katika wito mmoja wa madhabahuni. Wazia tu, hiyo ni, hebu tuone, thelathini, kumi, ishirini, thelathini, vema, hiyo ingekuwa karibu mara kumi ya ile idadi ya Pentekoste, uh-huh, hiyo ni kweli, karibu mara kumi ya ukubwa wa Pentekoste.

120 Ndipo kesho yake asubuhi meya akaniita, kwenye chumba changu cha hoteli. Akasema, “Ndugu Branham, nenda kwenye dirisha lako, upande unaoelekea ziwani, mara moja.”

Ndugu Bosworth alikuwa huko, kasema, “Ndugu Branham, ninakadiria . . . ”

121 Nami nikasema, “Sasa, ninyi mnaotaka kuombewa, mwaminini tu Kristo ninayenena habari zake.” Nami nikaomba ombi moja la kusanyiko, sasa, kulikuwa na yapata watu watatu tu jukwaani, nikaomba ombi moja la kusanyiko. Na ilikadiriwa, miujiza elfu ishirini na tano ya ajabu ilitukia mara moja.

122 Mnaona? Hawajajazwa kasumba: “Sisi ni—sisi ni Methodisti.” “Sisi ni Baptisti.” “Sisi ni Presbiteri.” “Sisi ni Umoja, Uwili, Utatu,” Na loo, mwajua, upuuzi huo wo—wote. Hawajui chochote juu yake. Walikuwa tu wakimtazamia Mungu aliyekuwa na Kitu fulani, ambaye angeweza kujibu. Mnaona?

123 Halafu, mnajua nini? Nilienda dirishani, nao wakishuka kwenye barabara hiyo, kama nitaishi kuwa na umri wa miaka mia moja na ningekuwa na akili zangu, kamwe sitasahau hilo, kukaja malori saba makubwa ya Uingereza, sijui ni nini, kama mnajua hayo ni nini au la, yenye urefu wa kutoka hapa kurudi kwenye ukuta ule, yaliyojaa mikongojo, mbao, viti vya magurudumu, vyombo, ambavyo walikuwa wamebeba kutoka misituni kwa mamia ya maili, na majuma kadhaa wakija, namna *hiyo*. Hayo hapo ndani yake, hayo malori saba ya mizigo, yamejaa hadi pomoni. Na nyuma ya hayo wakaja Wazulu, Wabasuto, Washangaani, Wahosa, na hao wote, nyuma yake, waliokuwa katika hivyo, vitu, siku moja kabla, wakishuka kuja barabarani, wakiimba katika lugha zao za kienyeji, “Amini tu, mambo yote yanawezekana.” Loo, ni saa ya jinsi gani!

124 Ninyi wanawake wa Canada hamfanyi hivi, bali nitasema hili kwa ajili ya kile Marekani ilicho. Wanawake wa Marekani wanafikia kiwango hivi kwamba, kila mwaka wanavua nguo zingine zaidi. Kufikia tu kwanza, nguo fupi, na sasa kufikia vitu vidogo vinavyoonekana kama nguo za wanaume, na vitu vya kuvalia. Ni fedheha, ni aibu, ni . . . ni—ni . . . Mwanamke fulani aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, mimi sivai kaptura,” akasema, “Mimi huvaa suruali ndefu.”

125 Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi. Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Hiyo ni kweli. Nami nikasema, "Hupaswi kufanya hivyo kamwe."

Kasema, "Vema, wao hawaninii...unapoenda dukani huwezi kununua kitu kingine ila hizo nguo za kizinifu."

126 Nikasema, "Siku moja utawajibika kwenye Kiti cha Hukumu kwa kufanya uzinzi. Huenda ukawa safi kama yungiyungi kwa mumeo; huenda ukawa safi kama yungiyungi kwa mvulana mpenzi wako. Lakini Biblia ilisema, Yesu alisema, 'Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.'" Nami nikasema, "Kama ukijianika huko nje na kuvalia namna hiyo, naye mwenye dhambi akuangalie na kukutamani, ni nani aliye na hatia, wewe au huyo mwenye dhambi? Naye atawajibika kwa jambo hilo, basi alifanya uzinzi na nani? Wewe. Ni nani aliye na hatia? Wewe, kwa kujianika namna hiyo." Nami nikasema, "Utakuwa na hatia ya kufanya uzinzi wakati huyo mwenye dhambi atakapowajibika kwa kufanya uzinzi."

"Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amezini naye." Ni nani aliye na hatia? Wewe. Hiyo ni kweli.

127 Mama huyu akasema, akaniandikia barua, akasema, "Bw. Branham, hawatengenezi nguo kama unazonena habari zake. Hizi ndizo aina pekee wanazoweka . . . "

Nikasema, "Lakini wangali wana vitambaa, tena wanauza cherehani," kwa hiyo hakuna udhuru kulihusu. Unaona? Hiyo ni kweli.

128 Sikilizeni, nataka kusema jambo hili, kumbukeni tu jambo hili, kama wakianza kuvaa kaptura huku Canada na kadhalika, mnaona, kama wakipata kufanya hivyo, kumbukeni tu hili: Hao wanawake wenyeji waliovaa blanketi, vijana kwa wazee, wasiojua mkono wa kulia wala wa kushoto, wamesimama pale, hawana kitu ila kitambaa cha shanga, uchi tu, mwilini mwao, walivyoweza kuwa, bila kujua walikuwa uchi, lakini dakika ile ile waliyomkubali Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi, walikunja mikono yao wapate kuondoka mbele za wanaume.

129 Basi niambieni ni kwa nini, kwamba kama watu hawa wanaojiita Wapentekoste, au Wakristo, au Wamethodisti, au Wabatisti, imekuwaje kila mwaka, mnadai kuwa na Kristo yeye yule, na Roho Mtakatifu yeye yule, na kujaribu kujianika zaidi kila mwaka? Kwa nini huyo Roho Mtakatifu amfanye mwanamke ajifunike apate kuondoka mbele za wanaume, na unapowaona kesho yake wamevaa nguo za namna fulani? Kwa nini awafanye wengine wavae nguo, na wengine wazivue? Mungu hafanyi kazi namna hiyo. Kuna kasoro mahali fulani, ndugu. Loo, jamani!

130 Hebu na tuondoke kwenye mawazo yetu ya kijamii na turudi kwenye Injili, amina, tuirudie ile kweli, turudi kwenye Neno. Si ajabu hatuwezi kuwa na Kanisa. Mungu angewezaje kamwe

kujenga Kanisa juu ya msingi kama huo? Hebu turudi kwenye kweli, ndugu, dada.

131 Samahani sana, ninapaswa kufanyiza mstari wa maombi sasa hivi, lakini hebu tuzungumze. Je, mna haraka? Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Samahani, ninyi jamaa, kwa kuchukua muda mwingi hivyo. Ninapata tu... Niliwaambia nilikuja hapa kupumzika, kwa namna fulani nina wasiwasi, nami nimekuja kupumzika, nami...Samahani.

132 Mungu Mtakatifu sana, moja kwa moja katika Uwepo Wako Mtakatifu na mbele ya kiti cha enzi cha rehema tunakuja, tukijikabidhi sasa. Sisi ni watu wasiostahili, Bwana. Wewe ni Mungu, uliyejaa rehema, uliyejaa wema. Uwe karibu nasi kutusamehe. Wakati moyo wangu unapowazia kuhusu Afrika, kuhusu India, Ee Mungu, jinsi ninavyowahurumia!

133 Ningewezaje kutumia makumi ya maelfu ya dola kwa ajili ya upumbavu, huku maskini watoto wadogo wamelala pale wakifa, na matumbo yaliyovimba, bila chakula? Ee Mungu, tusaidie kufahamu. Tungewezaje kuzunguka katika mlolongo wa Makadilaki, mapya kila mwaka, na vitu hivi vyote, na ndugu zetu huko wanahubiri Injili bila viatu miguuni? Watasimama katika Siku ya Hukumu, hivyo. Tunaweza kufanya nini? Sisi hapa, tukibishana kama tunapaswa kwenda kwenye kanisa *hili* ama *lile*. Loo, Marekani, Marekani, ni mara ngapi Yeye angewafunika?

134 Asante, Baba, kwa ajili ya Roho wa kweli wa Mungu, kwa ajili ya wakati huu wa ushirika kwenye hizo shuhuda, na pamoja na ndugu, katika maskini mahali hapa pazuri panapoitwa Grande Prairie. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya Waskandinavia hawa wazuri, Wajerumani, Wahindi, na kadhalika, ambao wamejitenga na mambo ya ulimwengu, nao wameyaweka wakfu maisha yao Kwako, wapate kuwa watoto Wako wapendwa, bila kujali ulimwengu utasema nini, bali wakiamini ya kwamba Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, wakijaribu kuishi vielelezo mbele za watu kusudi watu wote wapate kumwona Kristo ndani yao.

135 Tunakushukuru kwa ajili yake Baba, tunapolifungua Neno. Hakuna mtu anayeweza kulifungua, Bwana, ila tu...mtu yeyote aliye na nguvu za kutosha kuzifungua hizo kurasa angeweza kufanya hivyo, bali tunasoma katika Biblia ya kwamba kulikuwako na Mtu aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...uzima kwa mioyo yetu yenye njaa. Tunakuonea Wewe kiu, Ee Mungu. Kama ayala aoneavyo shauku kijito cha maji, nafsi yetu inakuonea kiu, Ee Mungu.

136 Turarue, ubinafsi wetu, ondoa u—ulimwengu kutoka kwetu, Bwana, na kutufanya Wakristo wazuri, wanyenyekevu, wapole, wanaomcha Mungu. Roho yetu imevunjika kabisa. Kwa hiyo

imeandikwa, "Yeye aendaye akipanda kwa machozi, bila shaka atarudi tena, akifurahi, akileta pamoja naye miganda ya thamani." Hiyo ndiyo shauku yetu, Bwana.

137 Bariki Grande Prairie, Bwana, wabariki wahudumu wake, wabariki watu wake, Mungu, ninaomba ya kwamba utawafanya malaika wa rehema, malaika wa Nuru. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaishi katika matukio ya kumalizia sasa. Hivi karibuni utakuja nasi tutamwona Yeye. Shida zote zitakwisha wakati huo. Mpaka wakati huo, Baba, utudumishe tumetiwa mafuta kwa upendo Wako na Roho Wako, ukitupa Mkate wa Uzima tupate kuwatumikia wengine. Ni kusudi hili tunaloomba mioyoni mwetu, katika Jina la Yesu. Amina.

138 Katika Kitabu cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 42, kwa muktadha mdogo tu.

139 Ninaona aibu kuwaweka hapa muda huu mrefu, lakini na—najua nina usiku mmoja tu zaidi. Nami na—naninii tu—natumaini tu tungekuwa na muda mrefu. Bado sijapata kuwahubiria. Kwa kawaida mimi—mimi huingilia tu shuhuda ndogondogo, kwa sababu, ndipo siendi kando, kama ukihubiri, umetiwa mafuta namna *hii*, upambanuzi uko *hivi*, unaona, nawe unajitikisa, mmoja kutoka kwa lingine.

140 Kwa hiyo ili kuzungumza tu nanyi kwa muda kidogo, ninataka kusoma se—sehemu ndogo ya Maandiko hapa kwa sababu maneno yangu yatashindwa, Maneno ya Mungu hayatashindwa.

> Na *malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosea: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

141 Ningependa kutumia hilo kwa ajili ya muktadha: *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa*. Kama wewe, unapoenda nyumbani, huenda ukasoma mlango uliotangulia na mlango huu.

142 Yesu alikuwa akiwakemea hawa Mafarisayo wa siku Zake, kwa sababu walikuwa wameshindwa kutambua Yeye alikuwa ni Masihi wao. Walikuwa wameridhika. Na watu wa siku hiyo, ilikuwa kabisa kama ilivyo siku hizi, ambapo watu walikuwa wakilitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu.

143 Sasa, ninatoa tamshi hili: Kama wewe ni Mkatoliki na unalitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu, umepotea. Kama wewe ni Mbaptisti na unalitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu, umepotea. Kama wewe ni Mpentekoste na unalitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu, umepotea. Lakini kama wewe ni Mkatoliki, Mpentekoste, ama Mbaptisti, ama chochote kile, nawe unamtazamia Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu, umeokoka. Kwa maana tunaokolewa kwa imani. Unaona?

144 Sasa, siku hizi watu wamefikia mahali ambapo wanalitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu. Kanisa halileti wokovu, wokovu ni wa Kristo. Mnaona? Kanisa halina wokovu, Kristo ana wokovu. Sasa, ningetaka kusema jambo hili, ya kwamba wanalitazamia kanisa kwa ajili ya wokovu, nao walipata nini? Kanuni za imani, na madhehebu, na—na kadhalika, na hilo ni jambo lile lile siku hizi. Kwa hiyo waliridhika kuamini ya kwamba hayo yalikuwa ni mapenzi makamilifu ya Mungu, wao kuwa na, na, kanuni hizo za imani, na kadhalika, na kufanya mambo hayo.

145 Kwa hiyo sasa, tunaona ya kwamba katika wakati huo Yesu alikuja, Jibu kamili kwa unabii wao kwamba alikuwa aje. Sasa, sisi sote tutakubali ya kwamba Yesu hakuja kinyume na Maandiko. Alikuja pamoja na Maandiko kabisa, lakini kinyume na vile makuhani walivyowaambia watu ya kwamba Yeye angekuja.

146 Sasa, manabii walikuwa wamezungumza juu ya, kwa mfano, Isaya, kasema, "Milima yote inarukaruka kama kondoo dume wadogo, nayo majani yanapiga makofi; na mahali palipoinuka pameshushwa, na mahali paliposhushwa pameinuliwa," wakati wa kuja kwa Yohana Mbatizaji.

147 Mbona, natarajia watu walidhani ya kwamba Mungu angefungua tu ushoroba, na kushusha vipandio vya dhahabu, ndipo nabii mkuu, mwenye nguvu, aliyevaa nguo za kuhani, angeshuka na kusema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani. Ndiyo kwanza nitoke kwenye ushoroba wa Mbinguni kumsalimia Kayafa hapa, na. . . " [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . kazi kubwa aliyofanya," na kwa makuhani mbalimbali, na kazi waliyokuwa wamefanya.

148 Hivyo ndivyo walivyokuwa wakitarajia jambo hilo, lakini lilitukiaje? Maskini mtu wa mwituni mwenye uso uliojaa ndevu za kipilipili alitoka nyikani bila ya. . . alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa, mwana wa Zakaria, alizaliwa mtoto wa kipekee, akatoka nyikani, akisimama pale, akiwakemea hao makuhani, na kusema, "Enyi kizazi cha nyoka nyasini, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo?" Whiu! Ni mtu tofauti jinsi gani! Mnaona?

149 Alikuwa nini? Amesimama matopeni kufikia kwenye vifundo vyake vya miguu. Amevaa nguo nzuri? Amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, amejifunga mshipi wa ngozi ya ngamia. Loo, jamani, jinsi alivyoitikisa hiyo mikoa! Alikuwa na Injili. Ilikuwa tofauti kabisa.

Nao wakasema, "Huyu ni mtu mshenzi, anayewazamisha watu majini. Naam, hapo, yeye ni—yeye ni. . . jamani, ni jamaa wa jinsi gani *huyo*."

150 Ndipo Yesu alipokuja, jina jeusi nyuma yake kama mtoto haramu, akiwa amezaliwa nje ya ndoa takatifu, aliyetengwa,

na kadhalika, Naye huyu hapa anakuja, akiitambua mioyo ya watu, na kuwaambia mawazo yao, na kutambua mawazo yao, na kufanya yale hasa Mungu aliyosema angefanya na manabii walisema angefanya. Ndipo wakasema, "Mtu huyu ni ibilisi." Um-hum.

151 Mnaona, wakasema, iliwabidi kuwajibika kwa kusanyiko lao, walikuwa wamesimama pale, wao, bila shaka Yeye alikuwa akifanya jambo hilo, kwa hiyo iliwabidi kufanya *kitu kingine*, kwa hiyo walisema tu, badala ya kulichunguza katika Maandiko, kama Yesu alivyosema wayachunguze Maandiko, "Yachunguzeni Maandiko, Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi," Yeye alisema, badala ya kufanya hivyo, walilijibu kusanyiko lao, "Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa pepo."

152 Sasa, kila mtu anajua ya kwamba mpiga ramli ni ibilisi, hivyo tu, ni roho wa ibilisi. Lakini mnaona, walikuwa wakimwita Roho wa Mungu roho wa ibilisi. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliwaambia hiyo ilikuwa ni kumkufuru Roho Mtakatifu na hawapaswi kamwe kusamehewa. Mnaona?

153 Sasa, na kwa hiyo alikuwa amefanya ishara hizi, nao walikuwa. . .Alikuwa akiwakemea, kwa sababu hawakuwa wameamini. Wa—walitaka kuninii. . .wa—wasingeweza kuamini, na hata hivyo Wayahudi waliamriwa kutafuta ishara ya namna hiyo.

Sasa, hivi Biblia haisemi, "Wayahudi wanatafuta ishara, Wayunani hekima"? Paulo alisema, "Nasi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa." Mnaona?

154 Wayahudi wangetafuta ishara, kwa sababu waliamriwa kufanya hivyo. Hiyo ndiyo sababu walikuwa wakifanya hivyo, kusudi wasimkose Masihi wao, mnaona, kwa sababu Yeye alikuwa awe Ishara kwa kanisa, kwa watu. Naye alikuwa amefanya yale hasa aliyopaswa kufanya, na hata hivyo hawakumwamini, kwa sababu ya mapokeo yao. Kwa hiyo Yesu alikuwa akiwakemea kwa kutokuamini kwao. Walipaswa kuliamini, bali hawakuliamini.

155 Nasi tunaona ya kwamba katika vizazi vyote, kila mahali, katika vizazi vyote, ambapo Mungu anatokea, ishara ya kimbinguni inakuja. Hakujapata kuwa na uamsho, mchukue Luther, Wesley, yeyote yule, uponyaji wa Kiungu na ishara kuu na maajabu yaliambatana na kila uamsho, kwa kuwa Mungu ni wa kimbinguni, na palipo na mambo ya kimbinguni, ya kimbinguni yatafanyika. Na sababu ya kuwa ya kimbinguni, ni kwa sababu Roho wa kimbinguni huwashika watu na kufanya mambo ya kimbinguni. Mnaona? Mungu ni Muumba, na kama Yeye yuko moyoni mwetu, mbona, Roho daima atasema, "Amina," kwa Neno Lake.

156 Sasa, katika Agano la Kale walikuwa na—walikuwa na njia mbili za kujua kama mtu alikuwa sahihi. Kwanza walikuwa

na sheria, kuna zile Amri Kumi. Lakini kama nabii alitabiri, halafu, mwotaji akaota ndoto, walikuwa na njia nyingine ya kujua. Haidhuru inasikika nzuri jinsi gani, mnaona, walikuwa na njia ya kimbinguni. Mungu daima alijithibitisha Mwenyewe. Msisahau jambo hili. Mnaona? Mungu hujithibitisha Mwenyewe kwa mambo ya kimbinguni, nyakati zote.

157 Ndipo hapa akaja mtu aliyekuwa nabii, naye akatabiri, na linasikika halisi sana kwa theolojia yake, lilisikika halisi sana hata lilikuwa kamilifu. Lakini mnaona, katika siku hii walikuwa wamekaa miaka mia nne bila nabii. Kwa hiyo wakasema. . . Walipata lundo la theolojia ya kujibunia. Sisemi hili kudharau, bali ndugu, hilo ndilo tuliloingilia tena, mnaona, wazo tu la kujibunia la jinsi kanisa linavyopaswa kuwa, vile Kristo anavyopaswa kuwa.

158 Si kuwa tofauti sasa, kama nilisema hilo kusudi tu niwe tofauti, basi Mungu airehemu nafsi yangu, ninapaswa kuwa hapa chini madhabahuni. Lakini sina budi kusema kweli. Mnaona?

159 Sasa, sasa angalieni, nao ndugu wahudumu wanajua hili, ya kwamba kama nabii alitabiri, ama, mwotaji aliota ndoto, haidhuru inasikika nzuri jinsi gani, walimpeleka kwanza kwenye, kile kinachoitwa, Urimu na Thumimu. Sasa, hiyo ilikuwa ni dirii ambayo Haruni alivaa, mawe kumi na mawili ya yale makabila kumi na mawili, yaliyotundikwa kwenye nguzo jengoni.

160 Walimpeleka huyu mtabiri, ama mwotaji huyu kule chini, naye akatabiri, ama—ama akasimulia ndoto yake mbele ya Urimu na Thumimu. Na kama nuru za kimbinguni zikianza kumulika, Mungu akitembea kati ya mawe haya kumi na mawili, ilifanya lundo la nuru kama upinde wa mvua, huyo alikuwa ni Mungu akisema, "Ni kweli." Lakini kama ninii, haikufanya hivyo, basi hawakuliamini. Haidhuru linasikika zuri jinsi gani, lilikuwa ni kosa.

161 Sasa, wakati huo ukuhani ulipoondolewa, ule ukuhani wa Haruni, ndipo hiyo Urimu na Thumimu ikaondolewa. Lakini katika ukuhani huu, ukuhani wa Melkisedeki, pia tuna Urimu na Thumimu. Haidhuru mhudumu anaweza kukwambia vizuri jinsi gani ya kwamba siku za miujiza zimepita, kwamba hakuna kitu kama kunena kwa lugha katika siku hii, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, hilo halitamulika kwenye Urimu na Thumimu ya Mungu, nayo Urimu na Thumimu ya siku hizi ni Biblia.

162 Kama Biblia inasema ndivyo ilivyo, unawezaje kusema ilikuwa tu kwa ajili ya mitume? Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili

yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Ninaweza kuwaonyesha dhahiri mahali ambapo Mungu alilipa Kanisa nguvu za kuwaponya wagonjwa. Sasa, mtu fulani anionyeshe mahali aliposema, "Sasa, nitazichukua." Nionyeshe hilo, mahali lilipo. Hakuna.

163 Zimo, nguvu zimo kanisani, bali kanisa limesahau jambo hilo, hawaziweki katika matendo, hawaziweki katika matendo. Kwa hiyo mnaona, imekuwa, tena, theolojia, theolojia ya kujibunia, na inapofanya hivyo, hailingani na Biblia ya Mungu.

164 Biblia ya Mungu ingali inabaki vile vile: "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Mnaona? Loo, ni, "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa ataishi; na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unasadiki haya?" Akasema.

Martha akasema, "Naam, Bwana nasadiki ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuja ulimwenguni."

Kasema, "Mmemzika wapi?"

165 Daima kuna, jambo fulani lilipaswa kutukia wakati imani halisi inapoletwa pamoja na Neno la Mungu. Kwa hiyo, ndugu, Neno la Mungu ni sahihi kila wakati. Lakini hao makuhani walikuwa wamelizungusha-zungusha na kufanya mapokeo, "Sisi ni Mafarisayo, tunaosha vyungu namna *hii*." "Sisi ni Masadukayo, tunaviosha *hivi*."

166 Loo, jamani. Ni kitu gani? Kuondoa moja, ni kama leo hii, "Mimi ni Mmethodisti juma hili, Mbaptisti juma hili, ninii . . . " Mnajua nini? Ni kama tu kuhamisha moja, maiti, kutoka chumba kimoja cha maiti hadi kingine. Hiyo ni kweli kabisa, naam, wanajiunga na makanisa.

167 Kwa nini usisahau jambo hilo na kuandikisha jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo Mbinguni? Hapo ndipo ambapo halitabadilishwa kamwe, hiyo ni kweli, limeandikwa kwa Jina na Damu ya Yesu Kristo Mbinguni, hapo haitambidi kulibadilisha kutoka kanisa hadi kanisa, jina lako.

168 Kuna Kanisa moja tu, Kanisa moja la Kikristo, na kuna njia moja tu ya kuingia Mle, si kupeana mikono, si kunyunyizia, si namna fulani ya ubatizo wa maji, bali kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuwa washiriki wa Mwili wa Kristo.

169 Sasa, lakini mnaona, wamechukua mapokeo yao na kuzitangua amri za Mungu. Yesu alikuwa akijaribu kuwaambia, "Nimekuja jinsi hasa nabii alivyosema ningekuja, wala hamtaamini." Na neno moja tu nyuma hapa, walisema, "Tungetaka ishara kutoka kwako. Tungetafuta ishara." Loo,

kila, kila kizazi Mungu amekuwa na karama katika Kanisa Lake.

170 Sasa, tunaona, kabla hatujalifikia somo letu, Yeye alirejea kwa Yona. Basi watu wengi daima wamewazia juu ya Yona kama mtu aliyekosa mapenzi ya Mungu; siamini ya kwamba mtu yeyote anayetembea katika mapenzi ya Mungu anaweza kuyakosa mapenzi ya Mungu. Siamini ya kwamba mtu yeyote anayetembea katika Roho anaweza kukosa mapenzi ya Mungu. Huenda akafikiri aliyakosa, bali Mungu huyafanya yote yatende kazi pamoja vizuri, Yeye huleta kila kitu sawa.

171 Baadhi yenu nyinyi wahudumu mmewazia, "Loo, jamani, kwa nini nimekuja mahali hapa? Vema nini kilitukia hapa? Kwa nini niliacha *hili*? Lakini nilijisikia kuongozwa kufanya hivyo."

172 Nilizungumza na maskini mhudumu mmoja leo, ndugu yuko hapa jukwaani, akiliacha kanisa na kwenda kwa Wahindi, ambako inambidi tu kwenda hapa na pale, popote awezapo, akiliacha kanisa zuri, kasema alijisikia kuongozwa kufanya hivyo. Nikasema, "Mwanangu, dumu na uongozi wako. Hiyo ni kusema, haidhuru kama inakubidi kulala kwa tumbo lako na kunywa maji ya matawi na kula biskuti kavu, nawe ilikubidi kubadilisha kuku mara tatu kwa siku, dumu katika mapenzi ya Mungu." Hiyo ni kweli, haidhuru gharama yake ni nini, dumu nayo, Mungu aliiita. Sasa, tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

173 Sasa, angalieni jambo lingine, basi tunaona ya kwamba Yeye alimrejea Yona, akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Yona, kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara; watapewa moja, kama ilivyokuwa katika siku za Yona." Sasa, Yona, tunajua, tunafikiri ya kwamba Mungu alimtuma huko Ninawi, lakini alishika njia akaenda Tarshishi, tunafikiri nabii alirudi nyuma, hakurudi nyuma.

174 Nilikuwa nikisoma jambo fulani juu yake, hapa, si muda mrefu uliopita, nalo likasikika ni zuri sana kwangu, na hivi ndivyo lilivyosema: Yona akapanda chomboni, halafu akatelemka, nao watu walidhani ya kwamba alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu, bali alikuwa katika mapenzi ya Mungu. Tunajua dhoruba ilitokea, nao wakaifunga mikono yake nyuma yake, na miguu yake, na kumtupa nje majini, naye Mungu akamfanya nyangumi mkubwa atokee, ama samaki mkubwa, na kummeza.

175 Na mtu yeyote anajua ya kwamba samaki anapokula, kwa kawaida huenda chini majini kisha anapumzisha pezi zake, vyaelea, pezi zake, chini ya maji. Hebu mlishe maskini samaki wako wa dhahabu uone kitakachotukia, akilijaza maskini tumbo lake, atashuka chini moja kwa moja, alaze maskini pezi zake chini, na—na kupumzika kidogo. Mnaona? Amelijaza tumbo lake, kwa hiyo a—anashuka tu kwenda kupumzika. Vema,

wakati nyangumi huyu alipolijaza tumbo lake kwa mhubiri, a—alishuka moja kwa moja, na, huko chini kabisa kupumzika.

176 Nami daima nilimhurumia Yona, mwajua, Yona, kama kuna mtu yeyote aliye na—na sababu ya kuzungumza kuhusu dalili!

177 Wengi sana wetu husema, “Vema, niliombewa, lakini ningali mgonjwa.” Hilo lina uhusiano gani nalo? Uliombwa kuamini, sio kuhisi, bali kuamini. Nawe unasema, “Vema, niliombewa, nilikuwa na mkono mbaya siku mbili zilizopita usiku, hakuna tofauti, nadhani niliukosa.” Vema, uliukosa hapo mwanzo. Unaona? Kama ungeliamini hapo mwanzo, kamwe usingejali hilo. Unaona?

178 Nena kuhusu dalili, Yona alikuwa na dalili! Angalieni hapa: Sasa, alikuwa huko chini katika tumbo la nyangumi, mikono imefungiwa nyuma yake, miguu imefungiwa nyuma yake, katika bahari yenye dhoruba, labda kipimo cha mikono arobaini kwenye kilindi cha bahari, katika tumbo la nyangumi, matapiko ya nyangumi yamemzunguka; aliangalia *huku*, kulikuwa ni tumbo la nyangumi, upande *huo* ulikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi. Hakuna mtu hapa aliye mbaya hivyo usiku wa leo, nina hakika. Loo, tumbo la nyangumi kila mahali alipoangalia.

Lakini mnajua yale aliyosema? Alikataa kuliona. Yeye akasema, “Ni ubatili wa uongo; lakini mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu, Bwana.” Loo, jamani!

179 Yona alijua ya kwamba wakati hekalu hilo lilipowekwa wakfu, kwamba Sulemani aliomba, na kusema, “Mungu, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote na wataliangalia hekalu hili takatifu na kuomba, basi, sikia kutoka Mbinguni.” Naye Yona alikuwa na matumaini ya kwamba mtu huyo alikuwa na imani katika Mungu, naye Mungu akayasikia maombi ya Sulemani. Naye Mungu akamdumisha hai mtu huyo siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi huyo, kisha akamweka mahali panapofaa. Kama aliweka tangi la oksijeni mle ndani, sijui alifanya nini, bali alimdumisha hai.

180 Na kama Yona, chini ya hali hizo, katika hali hiyo, angeweza kuangalia hekalu lililojengwa na mwanadamu na kuombewa na mwanadamu, ni zaidi sana jinsi gani sisi, usiku wa leo, chini ya hali hizi, tungeangalia mbali na hekalu, bali kwenye Kiti cha Enzi ambapo Mungu ameketi pale, na Yesu kwenye mkono Wake wa kuume pamoja na mavazi Yake Mwenyewe yaliyojaa Damu akifanya uombezi kwa ajili ya maungamo yetu, ameketi kama Kuhani Mkuu juu ya Kiti cha Enzi. Dalili hazimaanishi chochote kwetu basi, Mungu alisema hivyo na hilo latosha.

181 Yesu ameketi pale usiku wa leo kufanya maungamo yako sawa mbele za Mungu. Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri. Huna budi kuamini na kukiri, kwamba ndivyo

lilivyo, na ndipo Yesu anaweza kuanza kulishughulikia kwa ajili yako. Loo, naam.

182 Mungu alimdumisha hai siku tatu mchana na usiku. Nasi tunamwona basi. . .Tuliambiwa ya kwamba Waninawi wote walikuwa wamemwacha Mungu na kuanza kuabudu wanyama, ambayo ni tabia ya kikafiri.

183 Nao walikuwa, karibu kila mahali Ninawi, ulikuwa kwenye ufuo wa bahari, kwa hiyo kazi yao ilikuwa ni kuvua samaki, naye mungu wa bahari alikuwa nyangumi, yeye alikuwa ndiye kiumbe kikubwa kuliko vyote ba—baharini, na huyo alikuwa ni mungu wa baharini.

184 Siku moja yapata adhuhuri, wakati wote walikuwa huko nje wakivua samaki, maelfu yao wakivua samaki, mara akatokea yule mungu-nyangumi mkubwa, akakimbia ufukoni na kuutoa ulimi wake, naye nabii akatoka moja kwa moja kinywani mwake. Hakika, walitubu, bila shaka, mungu wa bahari alimleta nabii huyo moja kwa moja. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Kwa hiyo ilimbidi kumtia katika tumbo la nyangumi, hivi hamwoni?

185 Kwa hiyo Yona hakumkosea Mungu, hakumko-. . .a—alimjali Mungu. Mungu alifanya hivyo kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, akamwacha atoke kwenye kinywa cha nyangumi moja kwa moja akaenda ufukoni, na huyo alikuwa ni mungu akimleta huyo nabii, hakika wangemsikia.

186 Ninaweza kumwona akipitia mtaani, huku hicho kichwa chenye upara kiking'aa, akisema, "Tubuni, la sivyo katika siku arobaini mji huu utaangamizwa!" Mbona, waliwavalisha wanyama wao nguo za magunia; walitubu. Naam, bwana.

187 Loo, Yesu alirejea nyuma, na kusema, "Ninii kiovu na. . ." Nitaninii. . .Sikilizeni hili, kasema, "Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara." Kinatafuta ishara, kila mtu hana budi kuwa na ishara, "Huyu ana. . ."

188 "Kizazi kiovu na cha zinaa," Nitawaambia jambo moja, kama mtasikiliza kwa makini, mtaona kwamba alikuwa akizungumza kuhusu kizazi *hiki*, kiovu, kibaya na cha zinaa, kama Sodoma.

189 Nilikuwa Los Angeles, majuma machache yaliyopita, katika uamsho mkubwa kule pamoja na Assemblies of God, kwenye Ukumbi wa Manispaa huko Long Beach, nikachukua gazeti, na ushoga umeongezeka kwa asilimia arobaini, watu wenye matumizi ya kawaida ya maisha, waliopotoka. Tazama, mataifa yanaporomoka. Dhambi inatawala.

190 Wanafanya nini kwa. . .? Wamelifanyia nini Kanisa la Mungu wakati wote? Wamewacheka, na kuwaita watakatifu wanaojibingirisha, na walokole wa Kipentekoste. Watalijutia. Mataifa yatalijutia.

191 Mataifa haya yote hayana budi kuachilia, kwa kuwa Ufalme unakuja. Haleluya! Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali mlizoee sasa hivi. Naam, ninaamini hilo, kunakuja Ufalme na Mfalme. Loo, jamani!

192 Tunaona Yesu alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara," nao wataipata, watapata ishara, hicho ninii kiovu na cha zinaa . . . "kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa."

193 Kizazi hiki kiovu, cha zinaa kingepata ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo. Amina. Hilo ndilo tunaloona sasa, Kristo yu hai miongoni mwetu, ishara ya ufufuo, amina, Kristo wa Galilaya akifanya mambo yale yale, kazi zile zile pamoja na watu Wake, akiishi miongoni mwa wanadamu, akifanya ishara za Mungu aliye hai miongoni mwao.

194 Kizazi hicho kiovu na cha zinaa tunachoishi, kina ishara ya Yona, ule ufufuo, zile nguvu za ufufuo zinazoweza kumwinua mwenye dhambi kutoka katika maisha ya dhambi; zinazoweza kuwachukua wanawake wenye dhambi, wasioamini, waovu, waliopagawa na pepo, zikawafanya waaminio; zikawachukua wanaume duni na waliojishusha katika maadili, zikawafanya waungwana. Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, kizazi kiovu na cha zinaa kingepokea ishara, nayo ingekuwa ni ishara ya ufufuo.

195 Kumbukeni, katika ujumbe wa jana usiku, ama, jana alasiri, kwamba tunaishi katika siku za mwisho, katika ishara ya Uzao wa Ibrahimu kupata ishara ile ile ya mwisho. Nitamwomba mwanamume yeyote ama mwanamke aniambie ishara moja iliyoahidiwa katika Biblia nje ya ishara hii ya mwisho, aonyeshe mahali ilipokuwa. Jinsi ambavyo Ibrahimu, alivyoletwa kupitia kuhesabiwa haki, wakati wa Luther, utakaso, wakati wa Wesley, Roho Mtakatifu, wakati wa Kipentekoste, akithibitisha, akiweka karama katika ninii, Kanisa Lake, kisha akatokea huku amegeuza mgongo Wake, na kuyatambua mawazo ya Sara, huko nyuma, na nyuma Yake namna *hiyo*, na jambo lililofuata lilikuwa ni Moto kwa wasioamini, na kugeuzwa sura kwa mwili wa Ibrahimu, na hao, wapate kumpokea mwana aliyeahidiwa. Yachunguzeni Maandiko na mnionyeshe.

196 Tuko kwenye wakati wa mwisho, enyi kanisa, tuko kwenye mwisho wa safari, wenye kudhihaki, waovu. Samahani, si—sitaki kuwapigia makelele. Lakini wenye kudhihaki, ishara za wakati wa mwisho tunazoishi sasa, mioyo iliyopotoshwa, nia zilizopotoshwa, kinyume na Mungu. "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiowapenda walio wema." Mnasema, "Hao ni wakomunisti," hao ni wanaokiri kuwa Wakristo. Biblia ilisema, kifungu chenyewe kinachofuata, "Wenye mfano wa utauwa bali wakikana nguvu za Mungu,"

mnaona, "hao nao mjiepushe nao." Hilo ni la Kimaandiko. Aliliingiza katika ishara hiyo.

197 Halafu kinachofuata, tunaona, Yeye alirejea basi, kwenye wakati wa Sulemani. Kila kizazi Mungu amekuwa na karama, kote katika nyakati. Sasa, angalieni katika siku za Sulemani, ninyi nyote wasomaji wa Biblia mnajua, huo ulikuwa ndio wakati wa ufanisi sana kwa Israeli, Mungu aliwatumia karama, wakaiamini. Siku za Sulemani hakukuwako na vita, wote waliogopa, kwa sababu hao watu walikuwa na moyo mmoja, nia moja. Mungu alimpa Sulemani karama ya upambanuzi, nayo ilikuwa na nguvu sana, hata kila mtu katika Israeli, wote hao, waliiamini. Walijenga hekalu, hakukuwako na vita, nayo mataifa yakawatumia zawadi na kadhalika. Nitasema hivi, kwa sababu waliamini, nao umaarufu wao ukaenea kote ulimwenguni, na taifa lenye nguvu sana lililokuwako ulimwenguni.

198 Nitasema usiku wa leo kwamba Canada, Marekani, matumaini yetu hayajajengwa juu ya mahali fulani ambapo tungeweza kuingia kwenye kimbilio la bomu la kujificha kutokana na bomu la atomiki. Ungewezaje kamwe kuchimba lisikufikie? Mbona, yale tunayoyajua yatalipua shimo ardhini lenye kina cha futi mia moja na hamsini kwa maili mia moja mraba. Hayo ni yale tunayoyajua. Vipi kuhusu yale tusiyoyajua? Mbona, kama ukichimba futi elfu tano, ungeninii, vema, bila shaka, ungekuwa kwenye lava, lakini kama ungeenda futi elfu moja mia tano, mbona, mtikiso wa hizo ungevunja kila mfupa mwilini mwako. Hakuna njia kuyaepuka kwa kuyachimbia, saa imewadia.

199 Lakini tunalo kimbilio la bomu, halijatengenezwa kwa feleji, limetengenezwa kwa manyoya, "Chini ya mbawa Zake tutaishi." Bomu litakapoanguka, tutakuwa Utukufuni. Lakini mnaona saa hii imetufikia.

200 Sasa, vipi kama Canada yote, Marekani yote, sisi sote hapa pamoja, tungeiamini karama ambayo Mungu ametupatia, Roho Mtakatifu? Mbona, isingewabidi kuhofia Urusi. Mbona, mataifa yangetuogopa, Mungu angeweka hofu juu yao.

201 Alifanya hivyo alipoingia Palestina. Mnakumbuka kile Rahabu yule kahaba alichowaambia wale wapelelezi? "Hofu! Hatuna uhai uliosalia ndani yetu, kwa sababu tulisikia yale Mungu aliyowafanyia."

202 Mungu anaweza kufanya jambo lile lile, lakini tunajaribu kufanya nini? Kufanya mafanikio yetu wenyewe. Kwa nini usichukue njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo?

203 Ingekuwaje huko Canada usiku wa leo, kama kila mwanamume na mwanamke waliokiri kuwa Wakristo wangekusanyika pamoja na kuomba na kukubali ubatizo wa Roho Mtakatifu? Mataifa yangeiogopa sana Canada! Ni

watu wachache tu hapa, na hii milki kubwa mno mliyo ninyi, lakini mnge—mngeyafanya mataifa yawapigie magoti, bila shaka, mngeyafanya. Kwa sababu hatumkubali, hivyo tu. Katika siku za Sulemani wote walikubali.

204 Mngeweza kuwazia kila mtu akipitia Palestina akisema, "Loo, umewahi kwenda kanisani kufikia sasa?"

"Loo, vema, bila shaka, ninamwabudu mwingine."

"Haidhuru unaabudu nini,"

"Loo, nimesikia juu ya ninii yenu . . . "

205 "Njoo huku. Njoo uone karama kuu ambayo Mungu ametupatia. Loo, tuna ninii . . . Mungu wetu ni Mungu aliye hai, Mungu wetu ametupatia karama kuu. Mbona, iko juu ya mmoja wa ndugu zetu, tulimfanya mfalme. Nawe unapaswa kuja, uone karama hii, loo, ni kamilifu, ni upambanuzi, nao watu wanapitia hapa na kuiona."

206 Mbona, siku hizo, hawakuwa na televisheni, Bwana ashukuriwe, na kwa hiyo, ama, mambo kama tuliyo nayo siku hizi, na njia pekee wanayojua ni kuleta habari mdomo kwa sikio, na kupitia kwenye misafara wanapopitia nchini.

207 Na kila mahali watu wakipita katika uchuuzi wao na biashara, na kadhalika, wangeondoka, waseme, "Mnapaswa kwenda huko Israeli. Loo, mnapaswa kuona kile Mungu wao amefanya. Ameweka Roho Yake juu ya mtu, na mtu huyo ana hekima, upambanuzi. Lina nguvu sana hata hakuna kitu kinachoweza kusimama mbele zake."

208 Hilo lilikuwa ni jambo kuu jinsi gani. Loo, watu wangeshangaa. Mataifa yote yaliogopa, walituma maelfu ya kondoo na maksai, kila kitu, kufanya amani nao, "Hatutaki watu *hao* watukasirikie." Kwa sababu, mwajua, imeandikwa, "Ni afadhali jiwe la kusagia lifungiwe shingoni mwako, unajua, na kuzamishwa katika . . . "

209 Kwa hiyo hatimaye hilo neno likafika huko chini *kabisa* Sheba. Huko ni kuvuka Jangwa la Sahara, huko chini kusini, "Malkia wa Kusini," Yesu alirejea hilo. Ndipo akasema ya kwamba wakati maskini malkia huyu, kila mtu akipitia, na kupita, msafara huu mkubwa wa ngamia na kadhalika, wote wangesema, "Vema, mambo yanaendeleaje katika taifa *hili*?"

210 Kila mtu, "Vema, vizuri, lakini unapaswa kwenda Israeli. Loo, ndicho kitu kizuri sana ulichopata kuona. Mungu wao ameweka Roho Yake juu ya mmoja wa hao ndugu, na hao watu wako katika nia moja." Jamani, haya basi! "Kila Mwisraeli anamwamini Yeye."

211 Loo, laiti tungejiweka katika nia moja, tuweke mioyo yetu, si kwa sababu sisi ni Methodisti, Baptisti, Presbiteri, bali kuweka mioyo yetu juu ya hiyo karama, Roho Mtakatifu. Moyo mmoja: Wamethodisti waliamini, Wabaptisti wanaliamini,

Wapentekoste waliamini, Wapresbiteri waliamini, Katoliki inaliamini. Loo, jamani, si ingekuwa ni . . .? Loo, hiyo itakuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Hakika, nia moja.

212 "Kila mtu analiamini, unapaswa tu kuwaona. Loo, jamani, jinsi ambavyo Mungu wao humwaga hekima Yake juu ya mtu huyo! Hujawahi kuona kitu kama hicho, hakuna kitu kinachoweza kusimama mbele zake. Naye ni mwanadamu tu, bali ni Roho wa Mungu juu yake."

Vema, nini, imani huja namna gani? Kwa kusikia. Maskini malkia huyo anasema, "Hiyo ni kweli?"

"Naam." Imani.

Ndipo msafara mwingine ukapitia. "Mme—mmekuwa, aisee, ngojeni kidogo, mmekuwa Israeli?"

"Naam."

"Ni kweli?"

213 "Loo, ha—hakika ni kweli. Hujawahi kuona kitu kama *hicho* maishani mwako. Nilisimama mkutanoni kule siku moja, nami nikamwona mtu huyo akiwapambanua watu mpaka, ilibidi tu iwe ni kitu cha kimbinguni."

214 "Heri wenye njaa na kiu ya haki." Mnaona? Mnaona, imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu. Sasa, akaanza kuona kiu ya kwenda kujionea mwenyewe.

215 Sasa, kumbukeni, alikuwa na mengi ya kukabiliana nayo. Jambo la kwanza, yeye alikuwa ni mpagani. Sasa, ingembidi kushuka kwenda kanisani mwake na kupata ruhusa ya kuondoka. Hebu tuchukue, hebu tuambatane naye kidogo, mwasemaje?

216 Anashuka, anasema, "Mtakatifu kasisi baba, nimesikia ya kwamba kuna nguvu kuu za kimbinguni huko Israeli. Wana uamsho. Nao wananiambia ya kwamba Mungu wao ameweka Roho Yake juu ya mwanadamu, naye anafanya kazi ambazo mwanadamu hawezi kufanya. Haina budi kuwa ni Mungu wao anayefanya jambo hilo."

217 Ninaweza kumsikia akisema, "*Ahem*, *ahem*!" Yule askofu, mwajua, "Binti yangu, unatambua ya kwamba nyanya yako alikuwa mfuasi wa kanisa hili? Mama wa nyanya yako alikuwa mfuasi wa kanisa hili, mama wa nyanya yake alikuwa mfuasi wa kanisa hili, wewe ni mfuasi hapa, nawe ni mtu mwenye heshima, wewe ni malkia. Kamwe usijihusishe na kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha, uh, unajua, *watu*, ambao," samahani, "*kundi* hilo huko juu, kwa sababu wao kidogo . . . "

218 "Loo, lakini bwana, wananiambia ya kwamba, wao . . . Yeye, Roho wa Mungu wao yuko juu ya mwanadamu," mnaona, "na kwamba wao ni . . . na kwamba yeye hufanya kazi kama Mungu afanyavyo, kama Mungu wao."

"Vema, sikiliza, malkia wangu mpendwa, mimi ni baba-askofu wako, na kama kungekuwa na kitu kama hicho, kingetukia katika kusanyiko letu."

219 Mnajua hizo roho hazifi, zi—zinaendelea tu kuishi. Mnaona? "Kingetukia *kwetu* kama kungekuwa na kitu kama hicho, lakini kwa kuwa hakiko katika dhehebu letu, mbona, bila shaka, ni bure, ni mhemuko tu. Labda ni telepathia. Loo, tumesikia mambo kama hayo, bali ni uvumi. Usiyajali."

Hilo halikumridhisha, akasema, "Lakini, bwana, angalia, wananiambia ya kwamba ni Mungu aliye hai."

"Mpenzi, angalia ninii—angalia miungu tuliyo nayo hapa."

220 "Naam, hiyo ni kweli, vitabu vyote na miungu, lakini kamwe sijapata kuona chochote kikitembea ndani yao, Nyanya hakuona chochote kikisogea ndani yao, na nyanya yake hakuona chochote kikisogea ndani yao, wao si kitu ila lundo la maneno, wao si kitu ila lundo la sanamu. Lakini wananiambia *Huyo* ni Mungu aliye hai, anayeishi katika viumbe hai." Amina. "Ninataka kuona kitu halisi." Nautakia heri maskini moyo wake. "Ninataka kuona kitu ambacho kina uhai ndani yake, si sanamu iliyokufa, si theolojia rasmi iliyokufa."

221 "Ninamwamini Mungu, Baba, Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi; ninaamini katika Kanisa Takatifu la Katoliki ya Kirumi." Na kusema ati hiyo ni Kanuni ya Imani ya Mitume? Nionyeshe ni nini, Kanuni ya Imani ya Mitume huko nyuma katika Biblia. Hakuna hata neno moja kuihusu katika Biblia. Hiyo ni kweli. Ni nadharia ya kujibunia. Hakuna . . .

222 Mimi si, simaanishi kuwa katili sasa, na—nataka tu kuwaambia yaliyo kweli. Lakini kabla hujaweza kufanya ubao ushike, inakubidi kuupigilia, na kuupigilia msumari, nasi hatuna budi kuupigilia huu. Mnaona?

223 Yeyote aliyesikia kitu kama Kanuni ya Imani ya Mitume katika Biblia. La, ni upuuzi. Kanuni hizo zote za imani, hazikupeleki popote. Umezikariri kwa miaka mingi, na ungali unatangatanga katika dhambi na kupapasa-papasa gizani, wenye mfano wa utauwa. Na wakati Roho Mtakatifu anapofanya jambo fulani, mnaliita ibilisi. Mnajitia muhuri mbali na Mungu wakati wote. Hiyo ni kweli. Sikilizeni, ndugu na dada, msiwe hivyo, amkeni, tuko kwenye wakati wa mwisho.

224 "Loo," kasema, "Sasa, mpenzi, kama kulikuwa na miujiza yoyote ya kufanywa, kanisa le—letu lingekuwa nayo hapa." Hilo halikuridhisha. "Sasa, kumbuka, wewe ni malkia, wewe ni wa—wa Shirika la Rebecca, ama, jumuiya *nyingine*, wewe ni mwanachama wa Kiwanis, ama, unaona, huwezi kujihusisha na takataka duni kama—kama kundi hilo huko juu, unaona."

225 Ulitupiwa hilo usoni mwako. Mwanachama wa nini? Afadhali niwe mshiriki wa Mwili wa Mungu wangu kuliko

kuwa na mashirika yenu yote. Yatupeni kwenye pipa la takataka. Kweli! Mteteeni Kristo, "Juu ya Kristo, mwamba imara, nasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao." Chochote kinyume na Neno hilo, "Ne—neno la kila mtu na liwe uwongo," alisema Mungu, "na Langu liwe kweli." Hiyo ni kweli. Hakika. Neno la kila mtu na liwe uwongo.

Vema, maskini moyo wake ungali una njaa. Mwajua, kama una njaa, Mungu atakufanyia njia. Um-hum.

Baadhi yao walisema, "Usiendee hilo, hilo ni la Kipentekoste."

226 Inaleta tofauti gani? Mungu akinena na moyo wako, nenda hata hivyo. Haikubidi kumwuliza askofu kama unaweza kwenda au la. Mungu akizungumza nawe, ni nani atakayekuhukumu, askofu au Mungu. Unaona? Sasa, jambo la kwanza, mwajua, akasema, "Vema, nitaenda kwa vyovyote vile."

"Vema, tutaondoa jina lako kwenye kitabu."

227 "Vema, liondoeni tu." Hiyo ni kweli. "Nina—ninaenda, ninaenda, maana kitu fulani ndani yangu kinaona njaa." Loo, kilindi kinapoita kilindi, sauti ya maporomoko ya maji Yako! "Ninaenda kwa vyovyote vile."

"Vema, utaleta fedheha juu ya dini ya mama yako?"

228 "Ya Mama au si ya Mama, kuna kitu moyoni mwangu kinachoniambia niende nikajionee mwenyewe, sitasimama hapa nje na kulikosoa pamoja nanyi, nitaenda kujionea mwenyewe." Mungu aubariki maskini moyo wake. Hiyo ndiyo njia. "Nitanunua kila Gombo la Kiebrania la kila nabii aliyepata kunena. Nitaona jinsi Mungu wao alivyokuwa, na kama Mungu wao ni halisi na kujiweka Mwenyewe, kile alichokuwa kwa hao manabii, juu ya mtu huyo, nitasema, 'Yeye ni Mungu.'" Amina. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Yachunguzeni Maandiko, mwone kama Hayo ni kweli ama si kweli. Amina. Sijiitikii amina mwenyewe, bali *amina* linamaanisha "na iwe hivyo." Ni—ninaamini kwa moyo wangu wote.

229 Hapa, sasa, alikuwa na mengi ya kukabiliana nayo. Ninaweza kumwona akiwakusanya ngamia wake wadogo, na kundi lake la wasichana wadogo pamoja, kundi lake la matowashi na—na sasa akasema, "Unajua nini? Ninaenda kule juu, nami ninaenda kutafuta kujua. Na kama ni kweli, nitaiunga mkono." Kwa hiyo akawapakia ngamia wake dhahabu, na uvumba, na fedha, vitu vingi vya thamani. Sasa, yeye anasema, "Kama nikifika kule juu, na kama *ndivyo*, nitaiunga mkono. Kama *sivyo*, ninaweza kurudi na pesa zangu."

230 Hilo lingekuwa ni jambo zuri kwa Wapentekoste kujifunza, kuunga mkono vipindi kwenye tele-. . .kwenye—kwenye hizi redio hapa, ambao wangesimama huku, wacheke, na kukuita mtakatifu anayejibingirisha baadaye. Hiyo ni kweli. Msaidie

mchungaji wako, lisaidie kanisa lako, saidia huduma inayotetea jambo sahihi. Hiyo ni kweli.

231 Akasema, "Kama si sahihi, nitarudi na pesa zangu. Kama ni kweli, ninawiwa kitu fulani nalo." Hivyo ndivyo tunavyopaswa kujisikia. Ikiwa huyu ni Mungu, si pesa zetu tu, pesa zetu ni kidogo, bali tunawiwa Naye mioyo yetu, wakati wetu, vipawa vyetu, na kila kitu tulicho nacho, tunawiwa na Mungu. Kama ni kweli, hebu na tuingie ndani yake pamoja na kila kitu tulicho nacho. Kama si sahihi, nenda utafute iliyo sahihi, kisha uingie ndani yake.

232 Yesu alisema, "Kama nikitoa pepo, mnaweza kufanya hivyo kwa njia bora zaidi, njoni mfanye. Endapo mnaweza kulifanya vizuri zaidi, basi njoni mlifanye vizuri zaidi," Yeye alisema, "lakini kama natoa pepo kwa kidole cha Mungu, jueni Ufalme wa Mungu umewakaribia." Mnaona? "Sasa," Yeye alisema, "kama una njia bora kuliko Maandiko yasemayo, hebu tuone ukiitoa." Mnaona? Hiyo ni kweli.

233 Nilisema hayo katika chuo kikubwa hivi majuzi usiku, wakati mshauri wa chuo na hao wote walipokuwa wameketi pale, yeye hakujua, sasa, ni kama mtu yule, aliyeketi pale akiwazia hilo, hakujua ya kwamba nilikuwa nikilishika moja kwa moja jukwaani. Hakika. Aliketi kule nyuma akisema, "Loo, hakika ana . . . hakika ni mwanasaikolojia. Bila shaka yeye . . . "

234 Nikasema, "Basi kama mimi ni mwanasaikolojia, Mshauri, nakuomba uje hapa jukwaani na kuiendeleza ibada hii. Sina Ph.D. wala sijui lolote kuhusu saikolojia. Kama unayo njia bora zaidi ya kufanya hilo, basi njoo hapa," huyo mshauri wa shule. Nikasema, "Huyo hapo daktari wa saikolojia, njoo hapa ukalitekeleza, njoni, ninyi ni madaktari wa saikolojia. Lakini kama huwezi kulifanya, basi kaa kimya kulihusu." Kweli. Hiyo ni kweli. Ikiwa huwezi kufanya hivyo, huwezi kulifanya, nyamaza. Achana na Mungu. Kweli. Kwa hiyo, lilikuwa ni kundi tulivu sana.

235 Kwa hiyo tunaona maskini malkia huyo, aliandaa kila kitu apate kuondoka, naye akawapakia ngamia wake. Sasa, kumbukeni, alikuwa na mengi ya kukabiliana nayo, kumbukeni, katika siku hizo wana wa Ishmaeli walikuwa jangwani, nao walikuwa ni wanyang'anyi. Loo, ni mawindo rahisi jinsi gani kwa kundi hilo la wapanda farasi, kulivamia kundi hilo la walinzi wachache na kuwakatakata katika dakika moja, na maskini wanawake hao wachache pale, na kuwakatakata vipande vipande, katika kuvuka hilo Jangwa la Sahara! Ndipo basi wangefanya nini? Wajitwalie utajiri huo wote.

236 Lakini, mnajua, kama unamwonea Mungu kiu, kama unaona njaa, hakuna hofu njiani mwako. Unajua, wakati unapomwonea Mungu njaa, hakuna pepo milioni kumi wanaoweza kukuweka mbali Naye, ukimwamini Mungu, hakuna ibilisi anayeweza

kukushikilia, hufikirii juu ya hali ya mambo, una lengo moja, hilo ni kumwendea Mungu, amina, haidhuru ni nani anayesema lolote kulihusu. Loo, ingekuwa rahisi kwao. Lakini, mnaona, kama unaona njaa na kiu, utashibishwa, Mungu atahakikisha ya kwamba utafika kule. Kamwe hakuwazia chochote kuhusu hilo.

237 Safari ilikuwa ndefu jinsi gani? Pima ni umbali gani kutoka Palestina, ambako hekalu lilijengwa, kote kote chini mpaka mahali ilipokuwa ikulu ya huyo malkia huko Sheba, kupitia kwenye Jangwa la Sahara. Wala hakuvuka kule kwa Kadilaki iliyoyoyozwa, alivuka kwa ngamia. Inachukua siku tisini, miezi mitatu, juu ya mgongo wa ngamia, watu wengine hawatavuka barabara kuusikia. Magari, na ndege, na kila kitu, si ajabu Yesu alisema, "Atasimama katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki, alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu kusikia hekima ya Sulemani, lakini hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani," Yeye alisema. Bila shaka. Na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani usiku wa leo: Roho Mtakatifu, Mungu mwenyewe wa Sulemani. Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.

238 Alifanya nini? Baada ya kuvuka jangwa . . . alianza, kusafiri usiku, kwa sababu hiyo miali ya moja kwa moja ya jua hilo itakuchuna ngozi moja kwa moja, naye huyu hapa anapitia, hao ngamia, amepanda pale, akisoma hayo Magombo, kile Yehova alichokuwa. Amina.

Alipokuwa njiani ibilisi alisema, "Afadhali urudi."

239 "Nimekusudia kujua." Loo, ndugu, "Heri hao!" Hawa hapa wanakuja. "Sasa, tunaona ya kwamba Yehova hufanya jambo *hili*, Yeye alitokea katika manabii. Alifanya *hivi*; *hii* ndiyo njia Yake. Manabii walitabiri mambo. Huyu hapa mtu aliye na Roho yule yule wa upambanuzi, na kama *hilo* likifanya kazi, nitajua, nitaenda nione, nami nitaona kama ni kweli." Hatimaye akawasili langoni.

240 Sasa, yeye alikuwa tofauti na wanawake wa 1961, mnaona, toleo hilo lao, wanaingia, wanaketi chini kwa dakika chache, "Kama akisema jambo moja kinyume na kasisi wetu, tutaninii, tutaondoka mara moja." Hiyo inaonyesha ulilelewa vibaya. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Inaonyesha ulitoka kwenye nyumba ya namna gani. Unaona?

241 La, alikuja kukaa mpaka akaridhika kama ni kweli ama si kweli. Angeichunguza kwa Maandiko na kuijaribu aone kama ilikuwa ni kweli. Alikuja kukaa mpaka atakaposhawishika tena na tena.

242 Akapiga hema lake dogo, na kuwafungua ngamia mizigo, na kurudisha haraka pesa zake chini ya mahali hapo, na kuweka walinzi karibu. Kesho yake asubuhi, ninaweza kumwazia akitengeneza nywele zake vizuri sana, mwajua, na kuisafisha mikono ya—yake, na uso wake, na kuvaa vazi lake lililo bora

sana, naye anaenda kanisani. Anaketi chini, na be—bendi yote, baragumu ililia, na muziki ukachezwa, kabla tu ya kanisa kuanza. Ndipo baada ya kitambo kidogo, Mchungaji Sulemani akatokea, akaenda mimbarani, akaanza kuzungumza.

243 Basi mtu wa kwanza alipokuja, akasema, "Sasa, nitaona, ninajua Yehova ni nini hasa, Mungu wao, nitaona kama Yeye hufanya kazi namna hiyo. Anajua mawazo ya moyo, anajua siri za nia, kwa hiyo tutaona. Ninajua mtu huyo ni mwanadamu, ninamwona amesimama pale, amevaa nguo, yeye ni mwanadamu tu, kama mtu mwingine yeyote, kwa hiyo nitaona tu kama huyo ni Mungu ndani ya mtu huyo." Kwa hiyo jambo la kwanza, mtu alikuja jukwaani kwa Mchungaji Sulemani, naye akawaambia siri, akazifunua, ndipo maskini moyo wake ukaanza kurukaruka.

244 Jambo lililofuata, kesho yake, mengi zaidi yalisemwa, kesho yake, mengi zaidi yakasemwa, siku baada ya siku, na hatimaye kadi yake ya maombi ikaitwa. Na kwa hiyo, labda si hivyo, kwa vyovyote vile, mwajua, lakini aliingia kwenye mstari wa maombi, akasema, "Sasa, nitaona atakachosema atakaponifikia." Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo anaenda jukwaani mahali alipokuwa, "U hali gani?" Nayo Biblia ilisema ya kwamba hakukuwa na swali moyoni mwake asilojulishwa Sulemani. Amina. Ndugu, ilitenda kazi kwake wakati huo.

245 Alifanya nini? Akaligeukia kusanyiko, "Mimi ni Malkia wa Kusini, nimesikia kuhusu karama hii kuu ambayo Mungu wenu alimpa mtu huyu. Nami ninajua yeye ni mwanadamu tu, nilimpa mkono, nikamwangalia, yeye ni mwanadamu. Lakini kuna Roho juu yake, kwa kuwa hakunijua mimi, lakini Mungu amemfunulia yaliyo moyoni mwangu." Naye akasema, "Mungu wake anaweza kuwa Mungu wangu. Mambo niliyosikia kumhusu ni—ni ya ajabu, yote yalikuwa kweli, na zaidi ya niliyosikia." Kwa nini? Ilitenda kazi kwake, mnaona. Mnaona? Ilikuwa ni tukio lake mwenyewe. "Zaidi ya haya. Ni makuu kuliko niliyosikia." Naye akasema, "Hata heri watu walio pamoja naye wakati wote kuona kitu hiki kikifanya kazi, kwamba wamekuwa kule, heri hao watu." Kamwe asingemwabudu mungu mwingine ila Mungu huyo. Kwa nini? Alikuwa akiona njaa na kiu. Moyo wake ulikuwa umeridhika.

246 Yesu alisema, "Atasimama katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki cha Wayahudi na Mataifa, kwa maana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa." Loo, tumekuwa na yapata miaka elfu mbili mia tano ya mafundisho na ujuzi tangu wakati huo, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Roho Mtakatifu, Yesu Kristo katika umbo la Roho, akiishi katika Kanisa Lake, na kutimiza jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, akionyesha kufufuka Kwake kwa kizazi cha zinaa.

Alikuwa na shida gani? Kwa nini alisema hivyo? Sikilizeni, marafiki, katika kufunga, hivi. Alikuwa ameona kitu halisi.

247 Na mtu yeyote mwenye moyo mwaminifu aliye na akili timamu, na mwaminifu na mkweli, anataka kuona kitu halisi. Hilo ndilo ulimwengu unalotazamia siku hizi, si lundo la theolojia, si ya mtu fulani ambaye angeweza . . .

248 Yesu kamwe hakusema, "Vema, nisipotenda *mafundisho* ya Baba Yangu," Alisema, "Kama sizitendi *kazi* za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi aminini hizo kazi. Kama hamwezi kuniamini Mimi kama mwanadamu, aminini kazi nizifanyazo za Baba Yangu." Mnaona?

249 Aliona kitu halisi. Aliona kitu fulani, si lundo la kanuni za imani zilizoandikwa, bali aliona kitu halisi. Hicho ndicho watu wanachotaka kuona siku hizi, wenye mioyo miaminifu, kitu ambacho ni halisi.

250 Katika kufunga, nasema hivi, kila mtu anajua kwamba . . . Sisemi mimi ni mwindaji, napenda tu kuwinda. Mama ya mama yangu alitoka kwenye risavu za Cherokee. Kuongoka kwangu, tangu mimi . . . Pesa za kwanza nilizowahi kupata ni senti ishirini na tano, nikanunua mtego wa chuma, nikaanza kutega, nimekuwa katika hizo shughuli tangu wakati huo. Kwa hiyo ni—ninapenda tu kwenda peke yangu mwituni. Ninamwona Mungu mwituni. Kupanda milimani na kuketi kule, na kupanda juu kwenye kilele cha mlima, kuangalia kuchomoza kwa jua, na kusimama pale na kupiga mayowe mbele za Mungu.

251 Hapa wakati fulani uliopita, huko, huko Colorado, mimi ni kiongozi huko Colorado, nilifanya kazi kwenye ranchi kule, siku moja mimi na yule mwenye ranchi tulikuwa tumeenda kuwinda kulungu. Tulikuwa tayari tumewaingiza watalii wote ndani na nje, kwa hiyo tu—tukaenda kuwinda kulungu. Tukaenda huko nyuma kabisa ambapo wageni kwenye mazingira magumu, kama mnavyowaita "wageni," wasingeweza kwenda. Kwa hiyo tukapanda juu sana. Naye akaenda kwenye safu nyingine, nisingemwona kwa yapata juma moja. Nikamfunga farasi wangu wa matandiko. Ilikuwa kwa namna fulani, siku hiyo, ilikuwa ni msimu wa kiangazi, kulungu hawakuwa wamefukuziwa huko chini bado. Nami nilikuwa nimepanda juu sana kwenye mpaka wa msitu. Mvua itanyesha, na itaganda, halafu theluji itakuja, ndipo basi mvua itakuja, na halafu jua litawaka, mnajua jinsi ilivyo katika majira ya kupukutika majani.

252 Nilikuwa nikitembea pale, macho yangu yamefumbwa, nikisema, "Utukufu kwa Mungu! Wewe ni mkuu sana, Baba. Loo, Wewe ni mkuu *sana*. Huku juu sana peke yangu, ambako hakuna petroli wala sigara. Ee Mungu, si ajabu Wewe unaweza kuishi huku juu." Nikiendelea tu, kumsifu Mungu.

253 Muda si muda mwajua dhoruba ndogo ikatokea mlimani, nikaingia nyuma ya mti, kulikuwako na uwazi kule chini, ulikuwa karibu na mpaka wa msitu, nikashuka chini, nikashuka nyuma ya mti huu, nikaketi chini pale kidogo, ndipo dhoruba zikavuma kwa nguvu sana. Nilikuwa nimeinamisha kichwa changu namna *hii*, nikisema, "Mungu, Wewe ni wa ajabu, Wewe ni Mungu wa mlima, Wewe ni Mungu wa bonde, Wewe ni Mungu tunapokuwa maskini, Wewe ni Mungu tunapokuwa matajiri, Wewe ni Mungu tunapokuwa wagonjwa, Wewe ni Mungu tunapokuwa na furaha, Wewe ni Mungu ninapowinda, Wewe ni Mungu ninapolia, Wewe ni Mungu katika Mungu."

254 Nami nilikuwa kule, baada ya kitambo kidogo dhoruba ikapungua, nikaangalia kote, nikawaza, "Vema, Bwana asifiwe, dhoruba imekwisha, nadhani nitaendelea kuwatafuta kulungu wangu sasa."

255 Nikaanza kuondoka, na mara nikaangalia upande wa magharibi, kuelekea Canada, upande *huu*, jua kubwa lilikuwa limeingia kwenye mkoa huu hapa, nalo lilikuwa likipenyeza jicho lake kubwa kupitia mianya ya mwamba, nikaangalia kule, nikawaza, "Loo, naam, Yehova," nikaangalia nyuma hapa, na kulikuwako na upinde wa mvua, maana miti isiyokauka ilikuwa imeganda, mwajua, nao mwanga wa jua ukiiangazia ukasababisha upinde wa mvua kutokea kwenye bo—bo—bo—bonde. Nami nikawazia, "Huyo hapo, Yeye yuko hapa juu, Anaonekana kama jiwe la yaspi na akiki, Ufunuo 1, Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi, Yungiyungi la Bondeni." Loo, jamani, Huyo hapo, katika upinde wa mvua. Nikawaza, "Ee Mungu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Nami nikawaza, "Loo, ni ajabu jinsi gani!"

256 Yapata wakati huo, nikasikia maskini kulungu akilia. Chris, unajua ninalomaanisha. Nilisikia hiyo *mee-mee*, namna *hiyo*, nami nikawazia, "Loo, jamani! Alipotea katika dhoruba, alikuwa akiwaita hao wengine." Nikawazia, "Hilo hapo, kilindi, wanyama pori, wakiitana." Maskini mbwa mwitu wa kijivu akaanza kuita kilimani, mwenzake akamjibu huko chini. Halafu, ndugu, nawaambia, ile sehemu halisi ikanitoka. Nikasimama pale na kulia kama mtoto mchanga, Nikasema, "Ee Mungu, ni ajabu jinsi gani! Wewe huyo hapo katika upinde wa mvua, Wewe huyo hapo katika wito wa kulungu, Wewe huyo hapo katika wito wa mbwa mwitu, Wewe ni Mungu kila mahali! Loo, ni ajabu jinsi gani!" Nikasema, "Mungu asifiwe!"

257 Nami nikazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka huo mti, nikipaza sauti, kwa sauti yangu yote. Afadhali niwaambie ukweli. Nikapaza sauti, "Mungu atukuzwe! Haleluya!" Sikujali. Mtu yeyote anayepaza sauti kumfanya mtu mwingine amsikie akipaza sauti, hao ni mnafiki. Hakukuwa na mtu katika maili arobaini kutoka kwangu. Nilikuwa tu nikiruka

juu chini, nikikimbia kuuzunguka huo mti, nikipaza sauti, "Haleluya, haleluya, haleluya, Mungu asifiwe!" Ningeweza kumwona Mungu kila mahali, Yeye alikuwa halisi. Jamani, nami nikauzunguka mbio tena na tena. Vema, kama mtu angalikuja mwituni, wangedhani mtu fulani ametoka kwenye hospitali ya wendawazimu huko juu. Nilikuwa nikizunguka, sikujali, nilikuwa na wakati mzuri, nikitoa baadhi ya mvuke. Mnaona? Nilikuwa na wakati mzuri sana, nikisema, "Haleluya, haleluya!"

258 Ndipo nikasimama na kusema, "Ee Mungu, kwa nini nishuke kutoka kwenye mlima huu? Jamani, jalia niishi na kufia hapa juu, unizike hapa juu, unipeleke Nyumbani. Nitaweka bunduki yangu hapa, jalia mwanangu, Joseph, aipate siku moja, hebu awinde nayo, Bwana. Nitwae sasa, jalia niende." Loo, nikiwa tu na wakati mzuri sana. Kwa namna fulani sikuzote niliwazia, wakati mmoja nitapotelea mwituni. "Jalia—jalia niende, Bwana, nitoke, nitwaliwe kama Eliya alivyotwaliwa, nitumie farasi." Nilikuwa, loo, nikiwa na wakati mzuri sana pale.

259 Kwa ghafla nikasimama, na niliposimama, maskini, sijui kama mnao hapa ama hamna, naam, Chris, ninaamini mnawatega, maskini hao kuchakulo wa misonobari, loo, yeye ni polisi wa mwituni mwenye koti la samawati, kitu chenye kelele sana ulichowahi kusikia maishani mwako, si mkubwa vya kutosha kufanya chochote, aliruka juu ya kisiki na kusema, "*Kwe, kwe, kwe, kwe. Kwe kwe, kwe, kwe. Kwe, kwe, kwe.*"

260 Ndipo nikasema, "Sasa, ngoja kidogo, ewe jamaa mdogo," nikasema, "umesisimkwa hivi na nini? Kwani hukupenda hilo? Sasa, angalia hili!" Ndipo nikauzunguka, na kuuzunguka huo mti tena. Nikasema, "Ulipendaje hilo?" Mnaona? Nikasema, "Unapenda hilo?" Nikasema, "Unajua ninachofanya? Ninamwabudu Muumba wetu. Unapaswa kufanya jambo lile lile. Usinigombanishe." Nami ni—nikaendelea, nikasema, "Loo, laiti ungalimjua jinsi ninavyomjua. Yeye ndiye awapaye ninyi mbegu za misonobari. Mnaona? Aibu kwako! Usinisumbue ninapoabudu. Nyamaza!" Ndipo nikazunguka na kuzunguka mti huo tena.

261 Yapata wakati huo nikaona maskini jamaa huyo hakuwa akiniona. Maskini macho yake yalitokeza shavuni mwake, alikuwa amekodoa macho kichakani, namna *hiyo*. Nikawaza, "Kuna nini?" Mara tai mkubwa mno, aliyekuwa amelazimika kushuka kwenye dhoruba, akaja. Nikawaza, "Loo, hilo ndilo linalomsisimua, huyo tai." Upepo ulikuwa umempeperushia pale chini.

262 Nami nikawazia, "Vema, sasa, Mungu, mbona unikatize kuzungukazunguka mti huu hapa," ninaamini Mungu hufanya kila kitu kitendeke sawa, nikasema, "kwa nini Wewe unikatize kuzunguka-zunguka mti huu hapa kunifanya nimwone maskini

kuchakulo yule wa misonobari ama tai yule? Vipi kuhusu huyo tai? Maskini koho," nikasema, "mbona yeye ameketi pale kwa vyovyote vile?"

263 Nami nikamwangalia, nikawazia, "Vema, Mungu, hivi unaweza kuwa ndani ya huyo tai?" Nikamwangalia, nami nikawazia, "Naam, uko, kwa sababu haogopi." Hilo ni jambo moja, yeye hakuogopa. Nikamwambia . . .

264 Naye Mungu hataki mwoga, kama unaona aibu kushuhudia, usiende madhabahuni, unaona aibu kusema, "Kwa kupigwa Kwake mimi nimepona," unaona aibu kusema, "Naam, nilimpokea Roho Mtakatifu, haleluya!"

265 Mungu anataka kuweka uti wa mgongo, si mfupa wa shingo ya kuku, ndani yako, anataka kukufanya mtu fulani, kukupa ushuhuda. Kama vile Buddy Robinson alivyosema, "Nipe ushuhuda kama msumeno wa mbao. Weka maarifa mengi nchani mwa nafsi yangu, jalia nipigane na ibilisi mradi tu ningali na jino moja, kisha nimwume kwa ufizi mpaka nife." Na huo ulikuwa ndio ushuhuda wake, mzee Uncle Buddy, mwajua, na kwa hiyo alimaanisha hilo pia. Kwa hiyo basi, mwenye umri wa miaka themanini na mitano, angekimbia maili elfu sitini kwa mwaka katika gari dogo la Chevrolet, angali anahubiri Injili.

266 Aliandika kitabu, akauza nakala milioni moja, hakujua tofauti kati ya jina na kiwakilishi jina, kasema, "Sikuzijua, niliandika tu kitu hicho kwa ajili ya Bwana." Lakini alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu.

267 Sasa, angalieni huyu tai, niliwazia, "Kwa nini huogopi? Unajua nini? Ningeweza kuchukua bunduki yangu na kukupiga risasi." Bila shaka, alijua alinivutia kupita kiasi kufanya hivyo. Akaniangalia, nami nikawazia, "Vema, yeye haniogopi, maana alijua . . . " Nikamwangalia, aliendelea kuyajaribu hayo mabawa, mwajua, kuona kama hayo manyoya hayakuwa yakienda jinsi yanavyopaswa kwenda. Nikawazia, "Hakika, hiyo ndiyo sababu yeye haogopi, ana kipawa alichopewa na Mungu, mabawa. Naye ana imani katika kipawa hicho kilichotolewa na Mungu, alijua angeweza kufika kwenye msitu huo kabla sijaishika bunduki hiyo, a—alikuwa na imani."

268 Kama tai anaweza kuwa na imani katika mbawa zake, kama kipawa kilichotolewa na Mungu, ni zaidi sana jinsi gani tunavyopaswa kuwa na imani katika karama tuliyopewa na Mungu ya Roho Mtakatifu, kutubeba leo! Nikaangalia manyoya yake alipokuwa akisogea, nikawaza, "Vema, Ndugu, mimi ni . . . na—nakupenda sana siwezi kukupiga risasi." Unaona? Nikamwangalia.

269 Baada ya kitambo kidogo nikaona hakuwa na wasiwasi kunihusu. Alikuwa akimwangalia maskini kuchakulo huyo wa misonobari akipiga kelele, "*Kwe*, *kwe*, *kwe*. *Kwe*, *kwe*, *kwe*." Alitosheka nayo baada ya kitambo kidogo, akafanya tu mruko

mmoja mkubwa, labda alipigapiga mabawa yake karibu mara mbili, naye akaupita msitu huo moja kwa moja. Naye alipofanya hivyo, hapo ndipo nilipoona yale Mungu aliyokuwa akifanya. Jamaa huyo mkubwa hakupigapiga mabawa yake tena, alijua tu jinsi ya kuweka mabawa yake, ndipo kila wakati upepo ungeingia, angepanda juu yake. Baada ya kitambo kidogo akaendelea kupanda juu, juu, juu, pasipo kuusogeza unyoya, juu, juu, juu, mpaka akawa tu doa dogo.

Mimi huyo hapo, nimesimama pale, mikono yangu imeinuliwa juu Mbinguni, nikisema, "Loo, utukufu kwa Mungu!"

270 Jambo ndilo hilo. Sio, "*Kupigapiga*, *pigapiga*, mimi ni Mpentekoste leo; *pigapiga*, *pigapiga*, mimi ni Mbaptisti kesho; *pigapiga*, *pigapiga*, nitaenda kwenye mkutano wa Oral Roberts; *pigapiga*, *pigapiga*, nitaenda kwenye mkutano wa Ndugu Branham; *pigapiga*, *pigapiga*, nitaenda kwa Tommy Hicks." La! Ni kujua jinsi ya kuweka mabawa yako, mabawa yako ya imani katika nguvu za Mungu, kila wakati wimbi la utukufu linapoingia, panda juu yake.

271 Alimwacha maskini kuchakulo huyo wa ardhini ameketi pale, akisema, "*Kwe*, *kwe*, *kwe*. Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, hakuna kitu kama Roho Mtakatifu." Alichoshwa kumsikiliza, kwa hiyo akaweka tu mabawa yake na kuondoka. Loo, jamani, wekeni tu, jambo ndilo hilo, enyi marafiki, wekeni tu mabawa yenu katika imani.

272 Huko kwenye misitu ya kaskazini, nilikuwa nikiwinda pamoja na mvulana fulani, yeye ni karibu nusu Mhindi. Jina lake ni Bert Call, alikuwa mmoja wa wawindaji hodari sana niliopata kuwinda nao. Kamwe haikukubidi kumhofia Bert, popote mwituni, haikukubidi kumhofia, angeingia, namwchilia.

273 Nasi tulikuwa tunapenda kuwinda pamoja, lakini alikuwa ndiye mtu katili kuliko wote niliyepata kumwona; alikuwa na macho kama ya mjusi. Naye alikuwa akinicheka kwa kuwa ni mhubiri. Naye alikuwa ni jamaa mzuri, bali alininii tu—alininii tu—alikuwa tu na . . . alikuwa tu katili. Naye alikuwa anapenda kuwapiga risasi watoto wa kulungu ili tu kunifanya nijisikie vibaya.

274 Sasa, kumbukeni, ni sawa kumpiga risasi mtoto wa kulungu, hilo ni sawa, bali si kuwa tu katili, kumpiga tu risasi, kumwacha akae pale, na kulichekea hilo. Hilo ni kosa, hayo ni mauaji, mnaona.

275 Na kwa hiyo alizoea kusema, "Aa, mhubiri, wewe ni kama hao wengine, mwoga kupindukia. Ungekuwa mwindaji mzuri kama usingalikuwa mwoga sana."

Nikasema, "Bert."

Akasema, "Nilifikiri ulikuwa mwindaji."

Nikasema, "Mimi ni mwindaji, bali si muuaji. Unaona? Kuna tofauti kubwa sana katika hilo, Bert."

Akasema, "Aa, jirudie, Billy, jirudie. Sasa, ati usingempiga risasi mtoto wa kulungu?"

276 Nikasema, "Nimewapiga risasi watoto wengi wa kulungu." Nikasema, "Mungu, Ibrahimu alimchinja ndama na kumlisha Mungu, Naye akamla." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hakuna madhara kumwua mtoto wa kulungu kama sheria inasema unaweza kumchukua, ni sawa, lakini usifanye hivyo kikatili, kujionyesha tu. Kwa hiyo alifanya hivyo kusudi tu ajionyeshe.

277 Kwa hiyo siku moja nilikuwa huko juu, naye akasema, "Vema, Billy, umechelewa kidogo kuja wakati huu." Naye alikuwa na filimbi ndogo aliyokuwa ametengeneza, kisha akaichukua hiyo filimbi ndogo, naye angeipuliza, nayo ilisikika kama mtoto mchanga wa kulungu, huyo ni mtoto wa kulungu, akimwita mamaye.

Nami nikawaza, "Bert, hutafanya hivyo."

Akasema, "Aa, endelea, Billy."

278 Kwa hiyo sikuzote tulichukua jagi ya themosi iliyojaa chokoleti moto, maana inakupasha joto, ikitokea unageuzwa, kitu fulani. Samahani kwa kuchelewa, lakini nitafunga sasa hivi. Kasema, "Mimi . . ." Kasema, "Mimi . . ."

279 Tukaanza kutoka, na hao kulungu wenye mikia myeupe, loo, jamani, nena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, yeye alikuwa ni kuruta. Mnapaswa kuwaona wakiisha kurushiwa risasi mara moja. Loo, wanaweza kutoroka kama, unaona tu mahali walipokuwa. Na kwa hiyo, basi, wa—wao walikuwa wakienda kasi sana. Nao walikuwa wamefanya . . . msimu wa kuwinda ulikuwa umefikia majuma mawili, na, mbona, tulitembea asubuhi nzima, hata hatukuona mburuzo. Kufikia adhuhuri, kwa kawaida sisi huketi chini, kula chakula chetu cha mchana.

280 Kwa hiyo ilikuwa yapata adhuhuri, tukafika kwenye uwazi kidogo, yapata mara tatu ama nne ya ukubwa wa kanisa hili hapa, namna *hiyo*. Na kwa hiyo Bert akaketi chini. Wala hatukuwa tumeona mburuzo wala chochote. Na kwa kawaida tungetengana yapata adhuhuri, naye anashika njia moja nami ninashika nyingine, kisha tunarudi wakati fulani usiku huo kwenye kambi yetu ya miiba, ambako farasi wetu na kadhalika walikuwa.

281 Kwa hiyo basi wakati Bert alipoketi chini, alianza kunyosha mkono namna *hii* kifuani mwake. Nilifikiri alikuwa anataka kutoa themosi ya—ya—yake, mwajua, kutoa chokoleti yake. Kwa hiyo alipoanza kutoa kitu fulani, na ilikuwa ni ile filimbi ndogo, basi nikasema, "Bert, kweli hutaipiga hiyo."

282 Akasema. "Aa, mhubiri, jirudie," akaniangalia kwa macho hayo ya mjusi, mnajua, akachukua filimbi hii ndogo, naye akaipulizia, nayo ilisikika kama mtoto mdogo wa kulungu akilia.

283 Vema, nikashangaa, moja kwa moja ng'ambo ya pili ya mahali hapo kulungu jike mkubwa, huyo ni mama kulungu, akasimama. Alikuwa amejificha, mnaona, kichakani. Akasimama, hilo—hilo si kawaida. Huenda isiwe katika nchi hii, lakini ndivyo ilivyo katika ile nchi, uh-uh, si kawaida sana kwa kulungu jike kusimama, ama kulungu yeyote, wakati huo wa mchana, yapata saa tano.

284 Akasimama, akaangalia kote. Shida ilikuwa ni nini? Alikuwa ni mama, mtoto mchanga alikuwa hatarini. Akaangalia kote. Ninaweza tu kuona hayo masikio makubwa mno, hayo macho makubwa ya hudhurungi yakiangalia kote. Ndipo maskini Bert akanitazama kwa macho ya mjusi. Nikasema, "Bert, kweli hutafanya hivyo."

285 Kwa hiyo akaipuliza tena, naye huyo mama kulungu akatoka moja kwa moja kichakani akaingia kwenye uwazi. Sasa, hakuwa akiigiza chochote. Alikuwa ni mama, hicho kilikuwa ni kitu kilichozaliwa ndani yake, mama. Mtoto wake alikuwa hatarini, alikuwa akimtafuta. Akaangalia kote, akaenda kwenye uwazi.

286 Nilimwona . . . Kamwe hatubebi risasi ndani ya bunduki, tunapowinda pamoja namna hiyo. Kwa hiyo alikuwa na .30-06, akaivuta nyuma na, kwa urahisi sana na kuitupa hiyo risasi pale juu, wa punje ya uyoga 180. Naye alikuwa bingwa wa shabaha. Jamani! Nikamwona akisimama namna *hii* na kuelekeza mtutu wa bunduki kwenye moyo huo mwaminifu wa mama huyo.

287 Nikawaza, "Loo, jamani! Unawezaje kufanya hivyo, Bert? Unawezaje kufanya hivyo? Unawezaje kuwa katili hivyo? Katika dakika moja maskini huyo kulungu, moyo huo mwaminifu ndani ya mama huyo, hatakuwa na moyo wowote, utaulipua moja kwa moja umtoke." Mnaona? "Unawezaje kufanya hivyo, huku akimtafuta mtoto wake mchanga, huku ukimdanganya namna hiyo?"

288 Akatoka nje. Na wakati bolti iliposhuka kwenye hiyo ya mtindo '70 wakati iliposhuka chini namna *hiyo*, huyo kulungu akashtuka, akaangalia kote na kumwona mwindaji. Je, angeruka? La, bwana. Alijua alikuwa anakabiliwa na mauti, bali mtoto wake mchanga alikuwa hatarini. Akaendelea kusonga mbele, polepole, akimtafuta mtoto huyo mchanga, hayo masikio makubwa yameinuliwa juu, akiangalia, hiyo pua imeinuliwa juu. Akamwona mwindaji, naye alijua ilikuwa ni mauti katika dakika moja, hilo halikuleta tofauti yoyote kwake, mtoto wake alikuwa hatarini. Hakuwa akiigiza chochote, kama washiriki wengi wa kanisa wafanyavyo. Kulikuwa na kitu halisi, alizaliwa mama.

289 Akaangalia kote. Nikasema, "Siwezi kuliangalia." Nikageuza mgongo wangu. Nikasema, "Ee Mungu, usimwache afanye hivyo, usimwache alifanye, Bwana, kuna kulungu humu mwituni, usimwache amwue maskini mama huyo wa thamani, usimwache afanye hivyo. Ana mtoto mahali fulani la sivyo asingekuwa akifanya hivyo, anafikiri amepotea, anamlilia. Usimwache afanye hivyo, Bwana." Nikangojea dakika moja, nikisikiliza tu wakati wowote kusikia bunduki hiyo ikifyatuka. Nami nilijua kama ingefyatuka, hakika angekuwa kulungu maiti. Wala hakuwa amesimama yadi thelathini kutoka kwake, moja kwa moja kwenye huo uwazi.

290 Niliendelea tu kungojea, lakini hiyo bunduki haikufyatuka. Nilingojea, nikangojea, bunduki ingali haikufyatuka, nikawaza, "Kwani kuna nini?" Basi nikageuka, ule mshipa wa feleji katika ninii ya huyo nusu Mhindi . . . alikuwa akifanya *hivi*, akiitikisa namna *hiyo*, akageuka, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, akaitupa hiyo bunduki chini, akanishika miguuni, huku amesimama kwenye lile lundo la theluji, kasema . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

291 Huku macho yenu yamefumbwa, mkiomba, ni wangapi humu ndani wangetaka kuwa Mkristo wa aina hiyo ambayo huyo kulungu alikuwa ni mama? Ungetaka kuwa na upendo wa Kristo *sana* moyoni mwako, hata ungeweza kumwonyesha Kristo, si kitu fulani cha kujifanya, bali kuzaliwa *halisi*, kunakokufanya Mkristo, kama vile kuzaliwa kulivyomfanya huyo kulungu mama? Kama ungetaka kuwa na ujuzi wa namna hiyo, je, utainua mkono wako? Mungu akubariki. Mungu awabariki, kila mahali, bila shaka.

292 Baba yetu wa Mbinguni, hadithi hii ndogo rahisi, na hata hivyo watu wanajua ya kwamba wanakuhitaji, Bwana. Wanahitaji kuwa Mkristo, wanataka kuwa. Sote tunataka kuwa na kitu halisi ambacho tunaweza kuuambia ulimwengu kwamba Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu. Tujalie, Bwana, usiku wa leo, jalia tukio hilo limjie kila mmoja wetu.

293 Katika jengo hili dogo la labda watu mia moja na hamsini, zaidi ya nusu yao waliinua mkono wao kwamba walitaka tukio la namna hiyo. Bwana, inaonyesha ya kwamba hawana ujuzi wa namna hiyo. Naomba Kristo, usiku wa leo, katika utakatifu Wake mwaminifu, aonyeshe kusanyiko hili kwamba anawapenda, na anaweza kuwapa tukio hilo la kuwa Mkristo halisi, aliyezaliwa, si chochote cha kujifanya, bali tukio halisi. Tujalie, Baba. Kwa Jina la Yesu, Mwana wa Mungu, ninaomba.

294 Huku tukiendelea kuinamisha vichwa vyetu, kuna mtu hapa usiku wa leo, ama ni wangapi, hasa, ambao wangetaka kumkubali Yesu kama Mwokozi wako, na kusema, "Ndugu Branham, kama Malkia wa Kusini, na—nataka—ni—ninamtaka Kristo, kama mama kulungu, na—na—nataka kuwa Mkristo

halisi, sijawahi kuwa Mkristo, sijawahi kamwe, kamwe sijawahi kumchukua kama Mwokozi wangu, lakini usiku wa leo nataka kumchukua," waweza kusimama tu kwa miguu yako kwa dakika moja? Useme, "Ninataka kukumbukwa katika maombi."

295 Yesu alisema, "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu."

296 Waweza kusimama tu kwenye wakati huu? Useme, "Sijawahi kumtetea hapo kabla." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Simameni, wengine wenu, sasa. Mungu awabariki. Mtu mwingine? Simameni tu kwa miguu yenu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Mungu akubariki. Mtu mwingine, simama tu. Mungu akubariki, Dada. Mtu mwingine.

297 Amini tu, mwujiza mkuu kuliko yote ni wokovu, amini tu. Mmeona kitu halisi kuhusu Wakristo? Je, mtu fulani amefanya jambo fulani ambapo uliyaangalia maisha yao na kujua huyo hapo Mkristo halisi?

298 Wanne ama watano wamesimama, kunaweza kuwako na wengine kabla hatujafunga ibada? Mungu akubariki, ewe kijana mwanamume, jambo kuu sana ulilowahi kufanya maishani. Kunaweza kuwako na mwingine? Natumaini Mungu atapata mhubiri kutoka kwa mvulana huyo. Mtu mwingine?

299 Simama tu ama uinue mkono wako, useme, "Niombee binafsi, Ndugu Branham, mimi. . . Mungu anauangalia mkono wangu, kwa hiyo na—nakutaka uombe." Endeleeni tu, sasa, kwa muda kidogo tu, kila mtu akiomba, Wakristo wote wakiomba. Mungu akubariki. Mwingine? Aminini tu, aminini. Mungu akubariki, mwanangu. Ninamngojea tu Roho Mtakatifu.

Ee, Mungu, uturehemu.

Hebu kidogo, sasa. Ninii tu, ninangojea kwa dakika moja tu.

300 Baba yetu wa Mbinguni, tumengojea kwa muda kidogo tu, watu kadhaa wameinua mikono yao na wengine wamesimama kwa miguu yao. Maandiko yanasema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza; na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Jalia wajue ya kwamba hilo ndilo jambo kuu sana walilopata kufanya, lilikuwa ni kufanya uamuzi. "Yeye atakayenishuhudia mbele ya watu, huyo nitamshuhudia mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

301 Uturehemu Mungu, na uamini, tunaamini, kwa moyo wetu wote, ya kwamba utawaokoa watu hawa. Huenda kamwe nisiweze kuwapa mikono, lakini nitawapa katika Nchi ile ng'ambo ya mto.

302 Watume vijana hawa waende hudumani, Bwana, wafanye wahudumu. Hawa wote walioinua mikono yao na kusimama kwa miguu yao, wanaume kwa wanawake, tujalie, Bwana, jalia huu uwe ni wakati wa mabadiliko. Jalia kila wakati wanapofikiria

na kukutana na uovu, jalia wasimame kama yule mama kulungu wakiwa na ujuzi kwamba wanajua wamepita kutoka mautini kuingia uzimani.

303 Sasa, Wewe ulisema hivi, Baba: "Yeye, yeye alisikiaye Neno Langu," nasi tunaamini tumelisikia usiku wa leo, ingawa lilikuwa limevunjikavunjika, Bwana, katika njia yangu nyenyekevu ya kuliwasilisha, "yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna," wakati uliopo, "Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; bali," wakati uliopita, "amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ulisema hivyo, Bwana, ni—ninaamini tu Neno Lako. Ninamdai kila mmoja wao, ninawadai kwa ajili ya utukufu Wako. Sasa, tujalie, Baba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

304 Mungu awabariki. Jalia baraka nyingi za Mungu... Ninakuomba wewe uliyeinua mkono wako na kusimama, tafadhali, sitakuwa pamoja nanyi ila yapata siku moja zaidi katika uamsho huu, lakini wahudumu hawa hapa, kama unaishi karibu na makanisa yao, ambatana nao moja kwa moja, sivyo? Waendee, useme, "Mchungaji, nilikuwa kule kwenye kampeni usiku huo. Mimi ndiye niliyeinua mkono wangu. Mimi ndiye niliyesimama. Nataka unibatize katika ubatizo wa Kikristo. Ninataka uende pamoja nami na kutafuta mpaka tutakaponinii...nimejazwa na Roho Mtakatifu, na kupokea Ujumbe hu—huo walionena habari zake. Ninataka kitu halisi." Mungu awabariki.

305 Sasa, nitatumaini ya kwamba mtafanya hivyo. Najua mlilimaanisha. Na kama kweli ulilimaanisha kutoka moyoni mwako, hakuna pepo wa kutosha kuzimu wanaoweza kukutenganisha na Mungu. Umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Hilo ni Neno la Mungu Mwenyewe.

306 Ni karibu saa tano, tumechelewa sana kwa mstari wa maombi. Ninawaahidi ya kwamba kesho usiku, nitamwombea kila mtu aliye na kadi ya maombi, na kila mtu humu jengoni, anayetaka kuombewa. Nitafikiri hilo lingekuwa ni bora kidogo, kama si—sitahubiri tu ila—ila saa nne kesho, ama, dakika mbili tu kesho usiku, na kuanzisha mstari wa maombi. Je, mta—mtavumilia jambo hilo, kama nikiahidi kumwombea kila mtu kesho usiku? Fanyeni hivyo. Mungu awabariki.

Mnataka kuamini pasipo mstari wa maombi? Inamisheni vichwa vyenu.

307 Bwana Yesu, wako hapa. Nimehubiri tu juu ya kuona kitu halisi. Labda kuna wengine hapa ambao hawajawahi kukuona Wewe, Bwana, katika nguvu Zako kuu kufanya kazi. Ninaomba ya kwamba utawapa wanaume na wanawake nguvu na uweza sasa wa kuamini. Jalia walio wagonjwa, waliguse vazi Lako. Jalia niweze kuunyenyekeza moyo wangu kwamba Wewe

ungeitumia sauti yangu kuona ono la kuwaambia watu mambo wanayotamani. Tujalie, Baba.

308 Wakati mkiomba sasa, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu, macho yenu yamefumbwa, mkiamini kwa moyo wenu wote. Mwaminini Mungu. Endeleeni tu kuomba. Sasa, ninyi, kila mmoja, hatufahamiani, mbali na hawa watu wa Georgia na Ndugu Sothmann aliyeketi hapa. Mungu anaweza kutujalia hili. Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa na macho yenu yamefumbwa.

309 Kuna mtu aliyeketi hapa nyuma jengoni upande wangu wa kushoto. Ana ugonjwa wa wasiwasi, ana shida na mguu wake. Anamwombea mwanawe ambaye hajaokoka. Utaamini, ndugu yangu, na kukubali msamaha wako kutoka kwa Mungu, na shauku yako? Asante. Utaupokea.

310 Huyu hapa mama aliyeketi hapa, sijawahi kumwona hapo kabla. Nijuavyo mimi, hatufahamiani. Anaugua ugonjwa wa wasiwasi, pamoja na ugonjwa wa kike, amefanyiwa upasuaji, ana mkunjamano ubavuni mwake. Mtu fulani anaomba, maana ninaliona. Loo, kama hatalikosa! Unaamini, mama? Loo, ninawezaje kulipata?

Mungu, niambie yeye ni nani.

311 Bibi Fontane, simama kwa miguu yako. Hilo ndilo jina lako? Hiyo ndiyo hali yako? Hivi hatufahamiani? Basi Kristo anakupa shauku yako. Nenda, ukaponywe.

Alifanya nini? Mnaona kilicho halisi?

312 Huyu hapa mwanamume Mhindi anayeketi hapa, simjui. Mtu aliyesimama mbele yangu aliye na mkono uliolemaa. Unaamini Mungu atauponya huo mkono uliolemaa, Ndugu? Utaukubali? Mungu akubariki. Sikujua kamwe ulikuwa na mkono uliolemaa, bali Mungu alijua.

313 Unataka kuponywa hayo mawe ya nyongo? Sikujui, sivyo, bwana? Sina njia ya kujua hilo. Lakini hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili kusanyiko liweze kuona. Mshukuru Bwana.

314 Ninaamini ninyi Wahindi inawabidi kurudi, sivyo? Hebu hawa Wahindi waketi hapa, waniangalie. Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu?

Una shida ya kina mama, shida ya kike, kivimbe katika tezi ya kike. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, simama. Unaukubali uponyaji wako?

315 Mama huyu, hawezi kuzungumza Kiingereza, nanyi mnajua sijui hilo. Vema, zungumza naye kwa niaba yangu. Ana shida ya kiroho. Shida yake ni hii: anampenda Yesu lakini kamwe hajui jinsi ya kumwendea. Uh-huh. Um-hum. Anataka kutembea karibu zaidi na Yeye. Sasa, mwambie. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Utalipata. Mwambie. Mungu akubariki.

316 Baba, vipi kuhusu ugonjwa wako wa koo? Unafikiri Mungu atakuponya? Unaamini Yeye atakuponya? Kama unaamini, simama kwa miguu yako. Simama moja kwa moja, jambo ndilo hilo. Huyu Mhindi aliyeketi hapa akiniangalia, huku ameweka mikono yake katika ninii yake. . .namna *hiyo*, simama kwa miguu yako. Zungumza naye kwa lugha yake apate kuelewa. Vema. Umepata uponyaji wako. Nenda nyumbani, Yesu Kristo amekuponya.

Utaamini? Vipi kukuhusu wewe hapa ndani? Vipi kuhusu yabisi kavu? Unafikiri Yeye atakuponya? Simama na uukubali . . .?. . .Mungu akubariki.

317 Unaamini sasa? Kwa moyo wako wote unaamini? Usiwe na shaka, mwamini Mungu. Unaona jambo ambalo mwanadamu hawezi kufanya? Kila mmoja wa watu hawa ambao wameitwa, kama ninyi ni wageni, na mnajua ya kwamba sikujua shida yenu, inua mkono wako. Ninyi watu ambao mmeitwa usiku wa leo, inueni mikono yenu. Haya basi. Vipi kuhusu ninyi Wahindi, mnaojua ya kwamba sikujua shida yenu, mambo hayo ni kweli? Kama ndivyo yalivyo, yale yaliyosemwa, pungeni mikono yenu *hivi*, kila mmoja wenu, popote mlipo.

Vipi kuhusu hilo, mama? Unaamini kwa moyo wako wote, pia? Vema. Ilikuwa hivyo? Vema.

318 Sasa, mnaona ya kwamba ni Mungu? Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa, Roho Mtakatifu. Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, Yeye ni Mwokozi wako, Yeye ni Mponyaji wako, Yeye ni Mungu wako, Yeye ni Mfalme wako, Yeye ni Mkombozi wako, Yeye yupo hapa. Hivi hamwamini? Sasa, ni wangapi wanaompenda? Inua mkono wako. Loo, hilo ni ajabu.

319 Sasa, wengine wenu wekeaneni mikono, wekeaneni tu mikono. Chochote kilicho moyoni mwako . . .Kile ninachojaribu kuwaambia, mnaona, kwamba bila kadi za maombi, bila chochote, Mungu anajua hali yako, anajua yote kukuhusu. Sasa, ninyi ni Wakristo, ninyi ni waaminio, sivyo? Vema, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, usijiombee mwenyewe, mwombee mtu walioweka mkono wao, wa—wao wanakuombea, wewe waombee. Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Jinsi unavyoomba kanisani mwenu, hivyo ndivyo unavyomwombea mtu anayekuombea.

320 Baba yetu wa Mbinguni, saa zinaenda sana. Lakini Paulo alihubiri Injili ii hii usiku kucha, ndipo mvulana mmoja akaanguka kutoka dirishani na akafa, Paulo akaenda akaulaza mwili wake juu ya mvulana huyo, naye akafufuka tena.

321 Ee, Mungu wa Milele, Wewe uliyetoa ahadi, Wewe uliye wa kweli, Wewe ni wa milele, Wewe ni Yesu Kristo aliyefufuka, na leo katika wakati huu, wakati ulimwengu umekuwa kizazi kiovu na cha zinaa, unaona ishara ya Kristo aliyefufuka, pamoja

na watu wanaomwamini, walio na imani ya kutosha kumgusa, na kwa madhihirisho ya karama ya Kiungu, kunena kwa lugha ya kibinadamu kupitia mdomo usiostahili, na kuangalia kwa jicho lisilostahili, na kuona ono ambalo haliwezi kukosea kila wakati, Mungu yeye yule aliyetembea Galilaya, Yesu yeye yule aliyesema yule mwanamke angesimama katika Siku ya Hukumu, Malkia wa Kusini, na kukihukumu kizazi Chake kwa sababu alikuja kusikia hekima ya Sulemani, na kulikuwa na Mmoja pale akifanya kazi kubwa kuliko aliyofanya Sulemani, naye akaitwa Beelzebuli, na katika siku hii, Wewe ulisema, "Kazi hizi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya."

322 Wakati mmoja, mwanamke mmoja aligusa vazi Lako, Nawe ukageuka na kumtazama, na kumwambia, kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, imani yake ilikuwa imemwokoa. Ulisema ulikuwa dhaifu kwa sababu mwanamke mmoja alikugusa. Ningewezaje kusimama hapa kama mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, na kuacha dazani moja waniguse, na niendelee kusimama kwa miguu yangu? Ni kwa sababu Neno Lako liliahidi, "Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu."

323 Mungu, tunaishi katika siku ya kuona aliye mkuu kuliko Sulemani, Roho Mtakatifu, akidhihirishwa miongoni mwetu. Hawa hapa wanaume na wanawake ambao wameacha kila kitu ulimwenguni kukutumikia Wewe. Wamewekeana mikono. Hao ni watumishi Wako. Ninalaani kila ugonjwa, kila ibilisi.

324 Toka hapa, Shetani, umeshindwa vita. Waache, katika Jina la Yesu Kristo!

61-0515 Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa
Zion Gospel Tabernacle
Grande Prairie, Alberta Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org